# USOMEKAJI KATIKA FASIHI TAFSIRI:-
# UCHUNGUZI WA MATINI *MADHABAHU YA KILIO*

**NANGIRA, EUNICE. E**

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA M.A. KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library
0472590 9

**DESEMBA 2004**

## YALIYOMO

Ungamo ........................................................................................IV

Tabaruku ........................................................................................V

Shukurani ........................................................................................VI

**SURA YA KWANZA**

1:1 Utangulizi ........................................................................................1

1:2 Somo la utafiti ........................................................................................3

1:3 Madhumuni ya utafiti ........................................................................................4

1:4 Upeo na mipaka ........................................................................................5

1:5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ........................................................................................6

1:6 Uhalalishaji ........................................................................................12

1:7 Nadharia tete ........................................................................................14

1:8 Msingi wa kinadharia........................................................................................14

1:9 Njia za utafiti. ........................................................................................16

**SURA YA PILI:kaida za matini;upatanishi na muala**

2:1 Dhana ya usomekaji ........................................................................................18

2:2 Mwelekeo wa kihadhira........................................................................................20

2:3 Taratibu za kimatini ........................................................................................21

2:3:1 Upatanishi ........................................................................................21

2:3:2 Urejelezi / urudiaji ........................................................................................25

2:3:3 Marudio ya moja kwa moja ........................................................................................25

2:3:4 Usambamba ........................................................................................28

2:3:5 Viwakilishi ........................................................................................30

2:3:6 Udondoshaji wa maneno........................................................................................33

2:3:7 Njeo na hali........................................................................................36

2:3:8 Viunganishi........................................................................................39

2:4 Muala ........................................................................................41

2:4:1 Hali halisi ya maisha........................................................48

2:4:2 Lengo la mhusika...............................................................50

3:6 Hitimisho...........................................................................53

**SURA YA TATU**

3:1 Kaida za matini...................................................................54

3:2 Lengo la mtafsiri..................................................................56

3:3 Hali inayozunguka matini......................................................60

3:4 Yaliyomo...............................................................................64

3:5 Ukubalifu...............................................................................73

3:5:1 Kiasi cha yaliyomo...............................................................75

3:5:2 kaida ya ubora......................................................................78

3:5:3 Kaida ya uhusiano................................................................81

3:6 Mwingiliano matini.................................................................81

**SURA YA NNE**

4:1 Hitimisho...............................................................................89

MARAJELEO...............................................................................92

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya M.A katika chuo kingine chochote.

Nangira, Eunice E.

Tasnifu hii imetolewa kwa mtihani kwa idhini yetu sisi tulioteuliwa kuisimamia.

Zaja, O.
(Msimamizi)

KUTABARUKU

Kazi hii naitabarukia wanangu Grado Mabachi na Victor Mabachi walionipa moyo kila nilipoonyesha kutamauka pamoja na dadangu Lena Ajiambo aliyenifaa kwa mengi.Mbarikiwe kwa wema wenu usio kifani.

SHUKRANI

Kazi hii imekomaa kutokana na juhudi za watu mbalimbali, walionijali na kunongoza kwa njia kadhaa.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mawaidha na ushauri wao.

Shukrani maalumu nazitoa kwa msimamizi wangu Zaja Omboga aliyenishika mkono katika mwendo huo wote bila kuchoka. Alikuwepo kila nilipomhitaji kuhakikisha kuwa safari imetimia. Namshukuru sana.

Namshukuru Bw. Arege Timothy aliyenipa ushauri hapa na pale na kunihimiza nisikate tamaa.

Ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulishirikiana nao katika raha na karaha zetu katika safari hii; Jane Ochoki, Sussy Nandama, Sara Manzi, Evans Bogonko, J. Mutua, Duncan Kahiro na O. Odingo.

Pia nawashukuru marafiki zangu Mediatrix Mugadili, Asumpta Matei, Irene Omangi, Stella Amuhaya, Mary Waka na Lunar Odawa walionipa moyo na kunifundisha maana na thamani ya urafiki mwema.

Mwisho nawashukuru wazazi wangu Noah Sombo Wandera na Mama Lonar Apiyo Wandera. Kama si wao bila shaka nisingekuwepo kusomea shahada hii.Mungu awatunukie kila la heri katika maisha yenu.

# 1.0 SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

Umuhimu na uamilifu wa tafsiri katika mawasiliano na maingiliano ya kila namna, ni swala ambalo halipasi kuzua mijadala. Hii ni kwa sababu maingiliano na mahusiano ya kimawasiliano kati ya tamaduni mbalimbali yanawezeshwa kupitia kwa tafsiri. Hali kadhalika, tafsiri ni kiungo cha kimsingi na labda cha kipekee katika maingiliano ya kiitikadi, kiutamaduni, kijamii, kisiasa, kiuchumi na hata kielimu. Kwa sababu hii, tafsiri ni taaluma muhimu kwa jamii yoyote ile. Tafsiri ni taaluma ambayo umuhimu wake katika mijadala ya maswala nyeti katika jamii yoyote ile ni lazima uanze kutambuliwa na kupewa nafasi yake ya sawa katika kudadisi na kuielewa mienendo ya kimahusiano.

Katika maingiliano ya kiusomi na hasa sana usomaji wa fasihi, swala la tafsiri limekuwa ni swala la mjadala miongoni mwa wasomi. Hali hii inatokana na mielekeo mbali mbali inayotumiwa kuliangalia, kulishughulikia na kulijadili swala zima la tafsiri. Ipo mielekeo ambayo kimsingi huliona swala la tafsiri kama shughuli ya kuonyesha matatizo ya tafsiri na athari zake juu ya lugha na fasihi lengwa, japo mara nyingi athari hizo zinachukuliwa kimakosa kwamba ni lazima zijitokeze katika lugha na fasihi lengwa. Mielekeo hii hujishughulisha na kuonyesha makosa ya kiisimu yanayojitokeza katika tafsiri zilizokwishafanywa. Kwa mfano, kazi ya Wanza, A (1981), Zaja, O (1986), Ryanga C.W. (1986) na kadhalika. Lakini hata katika mielekeo hii, haijulikani wala haijapata kudhihirishwa ni kwa nini uorodheshaji huo wa makosa hufanywa. Pamoja na hayo, inakuwa kama kwamba uorodheshaji wa makosa haya unafanywa kwa ajili ya udhihirishaji tu, ikikumbukwa kuwa katika tafiti nyingi zilizofanywa kufuatia mkabala huu, makosa hayo hayajapata kutumiwa kufikia masuluhisho au mahitimisho maalum.

Pamoja na kwamba matatizo ya kiisimu hayakosi katika tafsiri yoyote, swali ambalo linahitaji kuangaliwa ni hili; ni kwa kiasi gani matatizo ya tafsiri, kuanzia yale ya kiisimu, kisarufi hadi yale ya maana na ufasiri, yanachangia au kutatiza usomekaji wa kazi zilizotafsiriwa? Swali lingine sawia na hili ni; Je, matatizo haya yanaweza kuzuia kazi iliyotafsiriwa kutoa mchango wa kifasihi katika fasihi pokezi? Ni kwa kiasi gani usomekaji unaweza kutumiwa kama kiungo cha kimsingi katika kuibua usomaji na ufasiri mpya tena tofauti na wa kazi iliyotafsiriwa? Haya ndiyo maswala ya kimsingi yanayochochea utafiti huu.

Azma ya kimsingi katika utafiti huu ni kuchunguza ni kwa kiasi gani usomekaji unachangia ukubalifu na ufasiri mpya au ufasiri badalia wa kazi iliyotafsiriwa. Usomekaji na ufasiri badalia ni mambo yanayotokana na mienendo ya sasa katika tafsiri, inayoshikilia kuwa si lazima kazi tafsiri iafikiane na kazi asilia kwa kila njia. Mienendo hii inathamini zaidi tafsiri zinazodengua na kuchengua kazi asilia kwa njia moja au nyingine. Pamoja na kwamba kazi tafsiri huchochewa na kazi asilia, kazi tafsiri haiwi kimelea cha kazi asilia kila wakati.Tutayatetea madai haya kwa kuichunguza na kuisoma kwa makini kazi ya tafsiri *Madhabahu ya Kilio* ambapo tunalenga kuonyesha jinsi kazi hii inavyosomeka na kwa hivyo kufasirika tofauti na kazi asilia *Shrine of Tears*. Tutajaribu kujihusisha na kunakidi mitalaa ya kisasa kuhusu tafsiri kwa vile inakwenda kinyume na mitazamo ya kijadi kuwa kazi tafsiri ni duni kuliko kazi asilia.Mitalaa hii inatambua kwamba kazi zinazotokana na tafsiri zinachangia pakubwa sio tu upanuzi wa hifadhi za kifasihi bali pia lugha na utamaduni wa lugha husika. Kama anavyosema Toury, G. (1995);

> Kazi za hivi karibuni katika taaluma ya tafsiri zimetilia shaka mtazamo wa muda mrefu kuwa matini tafsiri ni dhalili kuliko matini asilia (2).

Kutokana na misingi hiyo ya kuiangalia tafsiri, ni dhahiri kwamba usomaji na utafiti wa masuala ya tafsiri unajaribu kuiondoa na kuiepusha taaluma ya tafsiri na dhana tasa na hasi kuwa zipo matini za kifasihi za hali ya juu kuliko nyingine ati kwa sababu zilitungwa asilia. Matini zinaweza kutofautiana katika misingi ya ufundi uliotumiwa kuzifinyanga kazi zenyewe lakini mbinu za ufasiri na uhakiki wa kazi chanzi haziwezi kudaiwa kuwa zina uwezo wa kuibusha ufasiri na uelewa sawia katika kazi zilizotafsiriwa. Fauka ya hayo ni makosa kutarajia kwamba kazi tafsiri zitasomwa kwa njia sawia na ile ya kazi chanzi wakati ambapo mitazamo ya usomaji inazidi kubadilikabadilika kulingana na mpito wa vipindi maalum ambamo kazi husika zimeibuka.

**1:1 Somo la Utafiti**

Mitalaa katika somo la tafsiri katika fasihi ya Kiswahili imekuwa kwa kiasi kikubwa ikizingatia na kutukuza maandishi asilia; hata pale ambapo mitalaa yenyewe inahusu ufundishaji wa tafsiri au hata tathmini za kazi ambazo zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Mitalaa hiyo imekuwa pia ikijishughulisha na uhifadhi na udumishaji wa haki zote za kisanaa, kiutamaduni na za kiisimu za matini asilia. Haya ni mambo ambayo yanafanyiwa maamuzi bila ya kuwepo na usomaji wa kitaalamu uliojikita katika undani na upekee wa kazi iliyotafsiriwa au matini lengwa. Katika misingi hii, utafiti mwingi upatikanao katika fasihi ya Kiswahili kuhusu tafsiri za kifasihi kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili umeshughulikia matatizo ya uhamisho wa kazi hizo na udhaifu katika kazi za tafsiri zilizoko. Udhaifu huu kwa hakika ni jambo linalolazimishwa juu ya kazi zilizotafsiriwa kwa sababu kazi nyingi miongoni mwa hizo zimesomwa kutoka kwa mkabala wa kazi chanzi. Athari ya uhakiki na utafiti wa aina hii

ni kwamba una mahitimisho ya kijumla; mahitimisho ya kihisia yaliyo na mwelekeo hasi kwamba kazi zote za tafsiri ni duni na kwamba, kazi zote asilia ni bora na tukufu zaidi kuliko kazi zilizotafsiriwa.

Madai ya aina hii kwa bahati mbaya yana walakini. Hata kama kuna ukweli kuwa matini asilia ndicho kichocheo cha kuibushwa kwa matini tafsiri, hii si sababu tosha ya kuzuia kuchunguzwa kwa umuhimu, uamilifu na nafasi ya kazi zilizotafsiriwa katika fasihi pokezi. Kwa vile tafiti zilizotangulia zimekuwa zikipuuza swala la usomekaji, ambacho ni kipengee muhimu cha kuchunguzia uamilifu huo, utafiti huu unalenga kukishughulikia swala hilo. Pia ni lazima ikubalike kuwa matini pokezi ni kitu kipya na ambacho kinaweza kuwa na mchango mpya katika mfumo mzima wa fasihi na utamaduni pokezi. Ni kitu ambacho kinafaa na aghalabu hudai kusomwa na kufasiriwa kwa mujibu wa madai na matakwa ya lugha na fasihi pokezi.

Kutokana na maoni haya, utafiti tunaoulenga unakusudia kuchunguza usomekaji wa matini tafsiri ili tuonyeshe ni kwa kiasi gani fasihi tafsiri inachangia katika fasihi, lugha na utamaduni wa Kiswahili. Katika utafiti huu, ni muhimu ieleweke kwamba usomekaji unatumika hapa kama dhana iliyo na maana mbili. Kwa upande mmoja tuna maana ya usomekaji kwa mujibu wa madai na matakwa ya isimu; sarufi na sintaksia ya Kiswahili. Kwa upande wa pili, usomekaji umetumiwa hapa kwa maana ya ufasiri badalia kwa mujibu wa miktadha mipya ya kitamaduni na kiwakati ambapo kazi ya *Madhabahu ya Kilio* imezalika

## 1:2 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni makuu ya utafiti huu ni kuisoma na kuichunguza kazi ya *Madhababu ya Kilio* katika upekee wake kwa kujikita katika kipengee cha

usomekaji. Maswala makuu ambayo yataibuka kutokana na usomaji huu ni pamoja na:

1. Kuchunguza usanii katika matini tafsiri kwa kuisoma na kuifasiri kazi tafsiri ya *Madhabahu ya Kilio* kwa mujibu wa hali, dhamira, maudhui, ukabalifu na mwingiliano matini unaobainika katika mazingira yake ya Kiswahili.
2. Kuchunguza jinsi mtafsiri alivyotumia lugha ya Kiswahili katika miundo yake mbalimbali kwa mujibu wa upatanishi wa vipengee vya kiisimu na muala.
3. Kuonyesha jinsi uhalisi wa usomekaji wa kazi moja unavyoweza kutumiwa kutoa mahitimisho ya kijumla juu ya swala la fasihi tafsiri katika Kiswahili.

**1:3 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu unazingatia usomekaji katika fasihi tafsiri huku tukijikita katika usomekaji wa *Madhabahu ya Kilio.* Tunajikita katika vigezo mbalimbali vinavyotumiwa kupimia usomekaji wa matini ambavyo ni pamoja na taratibu za kiisimu, muala, lengo la mtafsiri, hali, yaliyomo, ukubalifu wa kazi na hali ya mwingiliano matini.

Kimsingi, utafiti huu utajikita katika ufasiri wa msomaji na kuchunguza mwitiko wake kwa mujibu wa mkabala wa kihakiki wa kihadhira, bila kuingilia mijadala ya nadharia za tafsiri wala uorodheshaji wa makosa ya tafsiri hii. Hatusemi kuwa makosa hayamo tunachokisema ni kwamba hata yakiwemo, tunayachukulia kama baadhi ya mifanyiko ya lugha katika harakati za kuiingiza matini husika katika utamaduni, lugha na mazingira ya

wapokezi kwa jumla. Kwa hivyo utafiti huu haujiingizi katika uorodheshaji wa makosa ya tafsiri kama zilivyofanya tafiti nyingi tangulizi.

**1:4 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili**

Swala la usomekaji pamoja na ufasiri katika kazi za kifasihi ni swala ambalo limeshughulikiwa kwa njia nyingi. Lakini mielekeo iliyopo na njia hizo mbalimbali zinaafikiana juu ya jambo moja; umuhimu wa msomaji katika usomaji wa maandishi kwa jumla. Kwa muda mrefu, imekuwepo mielekeo ya usomaji na ufasiri wa fasihi ambapo mwandishi hupewa umuhimu mkubwa kuliko msomaji. Mielekeo hii ya usomaji ni miongoni mwa sababu nyingi zinazoeleza ni kwa nini kazi asilia hutukuzwa zaidi kuliko kazi tafsiri.

Tukiizingatia matini tafsiri kama kazi yenye upekee wake, inabidi tuisome na kuifasiri kwa mujibu wa taratibu za lugha pokezi. Hii ndiyo sababu kazi ya Holbrook Jackson (1949) inatupa mwelekeo kwa jinsi ilivyoshughulikia nafasi ya kimsingi katika aina zote za usomaji. Maandishi yake yanaonyesha taratibu, mikakati pamoja na vipengee mbalimbali vikiwemo vya kifasihi vinavyohusika katika usomaji wa kitaalam. Vipengee vingine anavyoshughulikia ni pamoja na nafasi ya msomaji kama msanii, mikabala ya kusoma matini za kifasihi, wasomaji kama wahakiki na uhusiano kati ya mwandishi na msomaji kupitia kwa maandishi yanayosomwa. Kutokana na mambo haya, Jackson anafikia mahitimisho kwamba usomaji anaoufanya msomaji hautawaliwi na ufahamu au matakwa ya mwandishi. Msomaji yuko huru na usomaji na ufasiri wa kazi za tafsiri kama ilivyo katika kazi zozote zile za kifasihi, hutokana na juhudi za msomaji. Usomekaji basi, ni zao la kazi ya msomaji. Huu ni uelewa tunaokusudia kuuleta katika usomaji wetu wa kazi ya *Madhabahu ya Kilio.*

Swala lingine linalojitokeza katika utafiti huu ni swala la usomaji kiubaguzi. Hii ina maana kuwa usomaji wowote ule ni sharti utambue mambo muhimu kwa mujibu wa matarajio ya hadhira. Hii ni kwa sababu kuna mambo ambayo yanapuuzwa, kudondolewa au kubaguliwa kutegemea usomaji na mazingira ya usomaji yanayohusika. Hali kadhalika, hakuna usomaji unaoweza kujumuisha kila jambo kwa sababu kuna miktadha tofauti ya usomaji. Hili ni jambo lililo wazi katika usomaji wa kazi tafsiri kwamba kazi tafsiri husomeka katika miktadha tofauti sana na ile ya kazi asilia. Tofauti hizi huruhusu ubaguzi wa kiusomi ili kuafiki matarajio ya hadhira. Hili ni jambo ambalo tumelifuatilia katika utafiti huu. Ili kulibainisha zaidi, tumerejelea na kuazima maoni ya Thomson, D (1979) hasa kutoka mijadala aliyoifanya katika kazi yake ya *Reading and Discrimination* kuhusu usomaji wa kitaalam unaolenga kutambua na kubainisha mambo muhimu katika kazi ya kifasihi.

Mtazamo wa de Beaugrande, R na Dressler, W (1981) umeupa utafiti huu msingi sawa na ule wa Shreve na Nebert (1992). Wamezichunguza taratibu za kiisimu zinazochangia usomekaji wa matini kwa hadhira yake. Kazi yao inajadili taratibu hizi wakizingatia matini yoyote ile lakini utafiti wetu umeweza kuyaazima mawazo haya kwa kuwa, tafsiri huhitaji kusawiri taratibu hizi huku iking'ang'ania kutambulika kama matini asilia katika mfumo mzima wa utamaduni pokezi.

Swala la uitikio ni swala ambalo limepuuzwa au limepewa nafasi za pembeni mno katika tafiti zinazohusu fasihi tafsiri kwa mfano, Zaja, O (1986), Shitemi, N (1990), Mutie, E (1997) na kadhalika. Aghalabu katika tafiti hizi, kuna hali ambapo ufasiri wa kazi asilia unachukuliwa kuwa ufasiri sawa na ule wa kazi tafsiri. Inaelekea, watafiti wanafikia mahitimisho haya

kwa sababu ya kupuuza miktadha ya utunzi, hadhira na upokezi tofauti pamoja na uitikio katika mikabala mipya ya kifasihi na kitamaduni. Hoja hii ya uitikio inaoana na maoni ya Emmanuel Ngara (1982) juu ya usomekaji wa riwaya za waandishi wa Kiafrika. Si ajabu basi kuwa usomaji wetu umo katika mkururo huo wa usomekaji wa riwaya za Kiafrika. Tahadhari hapa ni kwamba, usomekaji wa riwaya za Kiafrika ni dhana jumuishi mno ambayo inaweza kuchochea fikra kwamba hakuna migao ya kiusomi na kifasiri katika usomaji wa riwaya za Kiafrika. Tofauti zipo, tena nyingi, ndio maana usomekaji wa *Madhabahu ya Kilio* ukahitaji mielekeo tofauti na ile ya *Shrine of Tears*, ilhali zote ni riwaya za Kiafrika. Ufasiri na usomaji wa kazi za kifasihi unaomtukuza mwandishi na kuiangalia hadhira kama kiungo cha pembeni umepata kupigiwa maswali ya kwa nini?

David Birch (1989) amelizungumzia swala la msomaji hasa kwa kumpa msomaji huyo nafasi za kimsingi katika kuibusha maana katika matini za kifasihi. Birch ameonyesha na kuzungumzia juu ya njia mbalimbali za kusoma, kuchambua, kuhakiki na kufasiri matini hizo. Katika njia hizi zote, Birch anaonyesha kuwa, usomekaji, kwa mujibu wa mkabala wa msomaji ni njia moja ya kimsingi ya kuhakiki na kufasiri matini za kifasihi. Swala la kimsingi analoliibua Birch ni kwamba maana ya kifasihi au hata ya kimatini inayojitokeza katika kazi maalum inatokana na ufasiri wa msomaji. Maoni haya yana mwelekeo unaofikiana na usomaji wa kazi za tafsiri tunaoukusudia, kuwa mtafsiri ni msomaji na mfasiri hivi kwamba usomaji wa kazi anayoiibua kutokana na tafsiri yake ni sharti utegemee miktadha mipya inamojitokeza kazi hiyo.

Birch ameshughulikia kwa undani uchanganuzi wa matini kwa kuzingatia mambo mbalimbali yaliyomo ndani ya matini inayosomwa pamoja na yale yanayoizunguka matini hiyo, bali yaliyo na athari za aina mbalimbali

kuhusiana nayo na jinsi inavyoweza kusomwa. Maoni haya yanachangia imani yetu kwamba, zipo njia pamoja na sababu nzuri za kuisoma kazi tafsiri pasina kufungika katika kazi asilia. Kama anavyosema Birch, usomaji, uelewa na ufasiri wa kazi asilia sio usomaji wa kipekee unaoweza kufanyiwa kazi tafsiri. Pili, kama anavyosema tena Birch, kila mara mtu anaposoma matini, upo uwezekano wa kuibua matini mpya. Hii ina maana kuwa ufasiri wa kazi asilia hauwezi kuwa sawa na ufasiri wa kazi tafsiri. Kila matini ina upekee wake hivyo usomekaji wao ni tofauti. Kwa kujikita katika uelewa huu pamoja na njia mbalimbali anazozipendekeza Birch, hasa njia zinazomjali msomaji, tunakusudia kusoma *Madhabahu ya Kilio* na kutambua kuwa usomekaji na ufasiri wake unawezekana katika lugha na fasihi ya Kiswahili pasipo kutegemea kuwepo kwa kazi asilia. Hali kadhalika tunataka kuonyesha kutokana na usomekaji huo kwamba mahusiano yaliyoko kati ya *Shrine of Tears* na *Madhabahu ya Kilio* ni ya kiutanzu na kinasaba na wala sio ya kifasiri.

Kwa njia kadha wa kadha, usomekaji katika kazi za kifasihi unaweza kuelezwa kuwa ni sawa na uteuzi wa wasanii. Yaani taratibu za lugha pokezi mathalan msamiati, miundo ya sentensi na mtindo kwa jumla ambazo mtafsiri anachagua kutumia ili kuwasiliana na wasomaji wake. Tunachomaanisha hapa ni kuwa, anachokisoma msomaji kinaongozwa na teuzi za aina mbalimbali. Baadhi ya teuzi hizo ni teuzi dhahiri na nyinginezo ni za kuhisika tu. Pamoja na hivyo, uteuzi ni sharti ufungike katika kazi iliyotafsiriwa. Hoja kwamba uteuzi unawezesha mawasiliano kutokea ni sharti iangaliwe kwa makini ili kuepuka ujumuishi potovu kwamba mawasiliano yanayowezeshwa katika kazi asilia ni sawa na yale ya kazi tafsiri. Vile vile, ikumbukwe kuwa usomekaji wa kazi asilia hauwezi kulazimishwa juu ya kazi tafsiri. Kwa mujibu wa maoni haya, utafiti huu utaliangalia upya swala la uteuzi kama

linavyoshughulikiwa na Shitemi, N (1990) lakini kwa tahadhari kwamba usomekaji wa kazi tafsiri unaathiriwa na aina tofauti za uteuzi; kwa hali hii uteuzi wa mtafsiri.

Shitemi anatoa hoja kwamba miongoni mwa mambo yanayochangia au yanayosababisha uteuzi wa visawe ili kuwezesha mawasiliano ni pamoja na maudhui, mazingira ya kiutamaduni, tofauti za kiisimu na hadhira lengwa. Jambo ambalo Shitemi haliweki wazi ni swala zima la hadhira – yaani haieleweki kama ana maana ya hadhira tu au matarajio ya hadhira hiyo. Katika usomaji wetu, usomekaji una mwelekeo wa karibu sana na matarajio ya hadhira. Hii inatokana na ukweli kuwa matarajio ya hadhira katika kazi asilia ni tofauti na yale ya hadhira ya kazi tafsiri. Katika misingi hii, kazi yetu itatofautiana na ya Shitemi kwa kuwa usomekaji unategemea uteuzi alioufanya mtafsiri, mbinu za kiisimu alizotumia kama viashiria pamoja na miktadha mipya alipoibusha kazi yake ya tafsiri.

Neubert, A. na Shreve, G (1992) wanajadili vipengele mbalimbali vinavyoipa matini yoyote ile mshikamano na udhabiti mwafaka unaoiwezesha kukubalika katika ulimwengu wa msomaji. Vivyo hivyo, matini tafsiri inaweza kukubalika kwa wasomaji wake na kupata hadhi ya kuwa matini yenye upekee wake ikisawiri vipengee hivi mbalimbali ambavyo huchangia matini. Mtafsiri ndiye kipatanishi kati ya maarifa yaliyo katika matini asilia na hadhira pokezi. Yaani mtafsiri hutambua matini yenye uhalisia unaoweza kuwanufaisha wasomaji anaowalenga kisha hutumia taratibu za kiisimu za lugha pokezi ili kuwasilisha ujumbe uliomo. Vipengele hivi vinavyoipa matini udhabiti ni pamoja na upatanishi wa taratibu za kiisimu kama vile usambamba, urejelezi, njeo na hali, viunganishi, viwakilishi na kadhalika. Vile vile sharti matini iweze kuonyesha waziwazi lengo la mtafsiri, hali inamozalika matini hiyo, yaliyomo, ukubalifu wake na mwingiliano matini

unaojitokeza. Mambo haya ndiyo yanayochangia usomekaji wa kazi hivyo ni sharti yapimwe kwa mujibu wa lugha pokezi, fasihi yake na hadhira pokezi kwa jumla. Hii ndiyo sababu utafiti wetu unaolenga kuchunguza usomekaji wa *Madhabahu ya Kilio* hasa kwa hadhira iliyolengwa na mtafsiri umenufaika na kazi hii.

Maswala haya yote ambayo tumeyajadili kufikia hapa yana mchango mkubwa katika kuelewa usomekaji wa kazi za tafsiri. Swala hili tutalifafanua zaidi hasa kwa kuafiki na kuzingatia maoni ya Gideon Toury (1995) kwamba tafsiri ni kanuni, uhalisi na ukweli wa utamaduni pamoja na hadhira lengwa. Kwa maoni ya Toury, tafsiri huchochewa na mahitaji ya fasihi pokezi, hulenga kuziba mapengo ya kifasihi au kitamaduni katika fasihi pokezi, kwamba fasihi tafsiri huibuka katika miktadha ya kifasihi na kiisimu ya lugha pokezi. Kwa njia hii, usomaji, uchambuzi, uhakiki na ufasiri wa kazi tafsiri hauna budi kufanywa, kuongozwa na kuafiki matakwa na matarajio ya lugha pokezi. Hivyo ndivyo ambavyo tumeisoma kazi ya *Madhabahu ya Kilio*. Kwamba hii ni kazi katika lugha na fasihi ya Kiswahili, ambayo usomekaji wake hauna budi kuafiki matarajio ya hadhira katika Kiswahili.

Swala lingine ambalo limejitokeza katika utafiti wetu ni swala la uitikio, yaani jinsi kazi za kifasihi zinavyopokelewa na kuitikiwa na kwa njia hiyo kupata ukubalifu katika hadhira inayolengwa. Hoja hii tutaitetea kwa kuazima maoni ya Joel Wingard (1996) kwamba kazi za kiubunifu na hasa kazi za utanzu wa nathari hubeba matukio na kwa njia nyingi huchochewa na matukio halisi ya maisha. Matukio haya mara nyingi huchukuliwa na mwandishi na kupangwa upya na kwa hivyo kupewa mwelekeo mpya. Upangaji huu mpya si jambo la sadfa bali ni jambo ambalo halina budi kujinasibisha na hali fulani halisi ya maisha. Hali hizo kwa upande wao huwa na athari juu ya jinsi kazi inayohusika inavyofasiriwa. Tafsiri nayo kwa

upande wake inaongozwa na mambo haya haya, yaani kuchukua kazi asilia, kuisoma, kuifasiri na kuielekeza upya ili iweze kujinasibisha na hali halisi za maisha katika mazingira na miktadha ya hadhira mpya ambayo ni hadhira pokezi. Ni dhahiri kwamba ufasiri na uelekezi mpya wa kazi zilizotafsiriwa ni matokeo ya usomekaji. Muhimu ni kukumbuka kuwa usomekaji huu unatokana pia na uitikio mpya, uitikio ambao hautawaliwi na uitikio uwezao kupatikana katika kazi asilia.

Hali ya uwingi lugha huchochea tafsiri kwa kiasi kikubwa. Lugha ndicho kiungo muhimu cha kupitisha ujumbe wowote ule na ni kipengee muhimu sana katika kuendeshea shughuli muhimu katika ulimwengu mzima. Hivyo, tafsiri inakuwa kiungo cha kimsingi kabisa katika kukuza lugha nyingine za ulimwengu ili kuweza kurahisisha mawasiliano katika ulimwengu. Huu ndio mtazamo unaochukuliwa na Shantha Ramakrishna katika makala aliyoiandika "Cultural Transmission Through Translation" (Sherry Simon na St. Pierre Paul 2000), anapolichunguza suala zima la tafsiri akizingatia mfano wa India. Mawazo haya yameipa kazi yetu msingi muhimu hivi kwamba tumeweza kuichunguza matini ya *Madhabahu ya Kilio* huku tukijiuliza maswali anayoyaibua Ramakrishna. Kwa mfano, tafsiri hii ya Kiswahili kutoka lugha ya Kiingereza ina misingi yake katika hali ya uwingi lugha katika nchi za Kiafrika au la? Huu ni mtazamo ambao umeupa utafiti wetu nguvu ya kuuhimili mwelekeo tuliouchukua wa kuchunguza hali inayoizunguka matini nzima pamoja na vigezo vinginevyo.

**1:5 Uhalalishaji**

Tumechagua kuitafiti na kuishughulikia mada hii kwa sababu zifuatazo: La awali ni kwamba, kazi nyingi katika fasihi ya Kiswahili ambazo zimeshughulikia swala la tafsiri zimekuwa na mwelekeo wa kujikita katika

uorodheshaji wa makosa ya kiisimu na kisarufi yanayojibainisha katika kazi tafsiri. Orodha hizi zimeelekea kutoa madai kuwa kazi tafsiri ni dhaifu. Hakuna kazi miongoni mwa kazi zilizochunguza swala la tafsiri katika fasihi ya Kiswahili ambayo imewahi kuuliza kama makosa hayo yamewahi kuzinyima kazi tafsiri usomekaji unaoweza kukubalika. Hili ni pengo ambalo linahitaji kushughulikiwa, na utafiti wetu unadai kwamba kila kazi iliyotafsiriwa ina uwezo wa kuibusha usomekaji wa aina maalum.

Pili, tatizo la makosa ya kiisimu na kisarufi ni tatizo dogo lakini kwa sababu zisizoeleweka limepewa kipaumbele sana katika usomaji, ufasiri na unakidi wa fasihi tafsiri ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi, kazi tafsiri nyingi hazipati nafasi ya kusomwa kihalisi yaani zisomwe kiutaalam katika upekee wazo. Kazi nyingi za tafsiri zimefanyiwa mahitimisho ambayo yamejikita katika usomekaji wa kazi asilia na sio usomekaji wa kazi tafsiri. Haya ni mahitimisho potoshi kwa kiasi kikubwa kwa sababu yanatokana na usomekaji unaolazimishwa juu ya kazi tafsiri. Hali hii inahitaji marekebisho yanayoweza kuonyesha kwamba kazi tafsiri zina uwezo wa kusomeka na kufasirika katika misingi ya upekee wao tofauti na kazi asilia. Tumechunguza uwezekano huu kwa kuisoma *Madhabahu ya Kilio* pasina kufungika katika *Shrine of Tears*.

Tatu, kila kazi tafsiri, hata zile zinazodaiwa kutafsiriwa vibaya zina michango kwa fasihi lengwa na michango hii haiwezi kupuuzwa. Njia moja ya kiuhakiki ya kubainisha michango hii ni kutambua usomekaji unaojikita katika kazi tafsiri pamoja na upekee wazo wa kimuktadha, kihistoria na kitamaduni. Hili ni jambo ambalo limepuuzwa na mielekeo iliyong'ang'ania uorodheshaji wa makosa ya kisarufi.

Nne, katika utafiti huu, tunaafikiana na kukubaliana na maoni ya Toury kwamba hakuna matini, hasa ya kifasihi inayoweza kudai au kusemekana kuwa ya kiasilia kabisa ambayo kwayo usomekaji na ufasiri wake ndio tu

unaofaa katika kila mazingira ya usomaji. Hili ni jambo linalochochea haja ya kuzishughulikia kazi tafsiri kwa kuchukua mtazamo tofauti unaozitambua kazi hizi kama kazi katika upekee wazo.

## 1:6 Nadharia Tete

1. Kuna uwezekano kuwa nafasi na uamilifu wa matini tafsiri ni mambo yanayobainishwa kwa kiasi kikubwa na fikra zinazochochewa na utamaduni wa jamii zinamotafsiriwa. Ubainifu huu ndio hupelekea matini tafsiri kukubalika katika jamii husika.
2. Matini tafsiri huweza kusawiri usanii unaokubalika katika fasihi na lugha ya hadhira lengwa hata isipoangaliwa kwa misingi ya matini asilia.

## 1:7 Msingi wa Kinadharia

Kazi tafsiri ya *Madhabahu ya Kilio* ambayo tumeamua kuisoma na kuifasiri ili kubaini usomekaji wake ni miongoni mwa kazi za kifasihi ambazo zimetafsiriwa katika kipindi cha baada ya ukoloni. Hii ndiyo sababu tumeonelea kuwa nadharia za tafsiri za baadaukoloni zitafaa kutupa mwongozo ulio na mashiko na unaoimarisha msimamo wetu.

Dhana ya baadaukoloni huhusishwa na mikabala ya kihakiki inayohusishwa na mataifa yaliyokuwa chini ya tawala za kikoloni. Nadharia hii ilizuka katika jitihada za majaribio ya kutaka kuzirekebisha hali fulani kuhusu jinsi mataifa ya kimagharibi yanavyoziona nchi zilizokuwa koloni zao. Katika kipindi cha ukoloni, watawala wa kiulaya walikuwa na mawazo duni kuhusu mataifa yaliyotawaliwa. Mtazamo huu ndio uliozikumba kazi tafsiri ambazo zilichukuliwa kuwa ni duni kuliko matini asilia. Yaani, mataifa yaliyotawaliwa yalichukuliwa kama miigo ya wakoloni. Basi mawazo haya ndiyo yaliyoiweka tafsiri katika nafasi ya chini katika hatua za kifasihi:

ikaitwa miigo ya kazi asilia. Sasa mitazamo ya baadaukoloni inatilia shaka mawazo haya.

Wananadharia wa baadaukoloni wameweza kuibuka na fikra tofauti ambazo kimsingi zinakosoa na kudadisi mielekeo hasi ya uelewa wa tafsiri. Fikira hizi ambazo kimsingi ni fikira za kibaguzi zinahitaji kuondolewa ili kuwe na uelewa wa mambo usiotegemea mielekeo ya kimagharibi. Maswala ya kimsingi yanayoshughulikiwa katika nadharia hii na yatakayotuelekeza katika usomaji na ufasiri wa kazi tafsiri ya *Madhabahu ya Kilio* ni pamoja na: je, tafsiri zimepewa nafasi gani baada ya mataifa haya kupata uhuru? Ni mikakati gani iliyochukuliwa na mataifa haya kuonyesha umuhimu wao na umuhimu wa utamaduni wao? Je waliwezaje kukabiliana na dhana ya kuitwa mwigo wa wakoloni huku wakitahadhari wasitupilie mbali kila kitu kilichotokana na ukoloni hata kile chenye faida kwao. Vilevile, katika tafsiri za kifasihi, nadharia hii inajaribu kuzipa matini tafsiri mwamko mpya ambapo uamilifu wake unatiliwa maanani hasa kwa kuziona kazi tafsiri kama vitovu vya utetesi wa kitamaduni.

Mwingiliano wa tamaduni unachunguzwa pamoja na umuhimu wa tafsiri katika kuziendeleza tamaduni za mataifa haya yaliyochukuliwa kuwa duni. Tafsiri inafaa kuibua kazi bora na inayoweza kufasirika kwa njia ya kipekee isiyotegemea kazi asilia, au kama itategemea kazi asilia utegemezi huo uwe ni kwa makusudi ya kuonyesha tofauti za kitamaduni, uelewa badalia wa mambo au hata kuonyesha jinsi kazi asilia zinavyoweza kutumiwa kuficha misimamo ya kibaguzi na kuendeleza uelewa wa kitaasubi. Katika utafiti huu tutachunguza ukweli wa mtazamo wa baadaukoloni kuhusu nafasi ya tafsiri, kwa kuchunguza vipengee hivyo.

Hata hivyo, dhana ya upungufu hasa upungufu wa kiisimu na kisarufi katika tafsiri bado inaendelea kushawishi mawazo ya wanafunzi wengi wa tafsiri. Karibu wote wanaanza na fikira kuwa lazima tafsiri iwe na upungufu na hivyo ni ya kiwango cha chini huku wakisahau kuwa hiyo tafsiri huenda ina faida zaidi. Lakini nadharia za baadaukoloni zinapinga kuwepo kwa matini za hali ya juu kuliko nyingine kifasihi. Ni kweli kuwa zipo matini zinazothaminiwa zaidi ya nyingine lakini ikumbukwe kuwa mikakati ya kutathmini inabadilika kila uchao kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Hii ndiyo sababu utafiti wetu ukajinasibisha zaidi na kuchunguza usomekaji wa kazi husika bila kujiingiza katika uorodheshaji wa makosa ya tafsiri.

Sasa, uzito wa tafsiri unaegemezwa kwa mtafsiri na si mwandishi wa matini asilia kwa jinsi inavyochukuliwa kuwa tafsiri pia ina upekee wake kama matini. Huu ni mwelekeo tofauti na ule unaomzingatia mwandishi wa matini asilia na mtafsiri kuchukuliwa kama mtumwa wa matini hiyo. Kulingana na nadharia za baadaukoloni, tafsiri ni mawasiliano ambapo mtafsiri ni msomaji muhimu na mwenye uhuru kama mwandishi. Kwa kufuata vipengee hivyo tulivyovijadili vya nadharia za baadaukoloni, tutaisoma na kuifasiri *Madhabahu ya Kilio* ili kuibusha usomekaji kwa misingi ya muktadha ambamo kazi hiyo ilizalika.

### 1:8 Njia za Utafiti

Tumesoma kazi mbalimbali maktabani ili kujenga msingi imara wa kinadharia ambamo utafiti huu utaendelezwa. Pia tumezungumza na wataalamu mbalimbali katika uwanja huu wa tafsiri na fasihi na wameweza kututolea maoni yao kuhusu mada yetu. Tumesoma riwaya za *Shrine of Tears* na *Madhabahu ya Kilio* kwa umakini sana ili kuweza kuchunguza usomekaji wazo.Kwa kusoma vitabu vinavyozungumzia kazi tafsiri, tumeweza kufanya

mijadala mbalimbali na wanafunzi wa Kiswahili ili kubaini usomekaji wa matini hii kwa upekee wayo.

# SURA YA PILI

## KAIDA ZA KIMATINI: MSHIKAMANO NA MUALA

Katika sura hii tumeshughulikia kaida mbili muhimu zinazoipa matini yoyote ile uthabiti mwafaka. Vipengele hivi ni pamoja na vipengee vya kiisimu vinavyoipa matini mshikamano unaofaa na muala (mfuatano wa matukio pamoja na mawazo katika matini) ili kuwezesha usomekaji wa kazi husika.

### 2:1 Dhana ya Usomekaji

Usomekaji kama unavyotumika katika utafiti huu, ni dhana iliyo na maana mbili. Kwanza, tunautumia usomekaji kwa maana ya matumizi, ukamilifu, utimilifu na uwiano wa vipengele na sheria za kiisimu na pili kwa maana ya ufasiri wa matini husika kwa mujibu wa yaliyomo na jinsi yanavyotambulika na yanavyokubalika katika mazingira halisi ya wasomaji wa mfumo pokezi. Huu ni mwelekeo wa kumzingatia msomaji ambaye si mfukuzi wa maana iliyoko katika matini chanzi bali mhusika hai anayeunda na kufasiri upya matini anayoisoma kwa mujibu wa matakwa na matarajio yake ya kiusomi. Kwa hivyo, msuko wa matini unaathiri usomekaji wa matini yoyote kwa kiasi kikubwa. Msuko unatumiwa kwa maana ya vipengee vya ndani ya matini kama vile miundo ya kiisimu na vile vile miundo ya kiitikadi, kifalsafa, kiuchumi na kihistoria inayochangia kuibuka matini hiyo.

Usomekaji vile vile unahusu jinsi kazi fulani inavyomvutia msomaji kwa jinsi inavyoeleweka na kuleta maana katika ulimwengu wa msomaji huyo. Mawazo haya kwa mujibu wa maoni ya Ngara, E (1982:22), yanatambua kuwa usomekaji unahusu pia mwingiliano wa mifanyiko

mbalimbali ya kimtindo. Mtindo wa mwandishi kama ulivyo mtindo wa mtafsiri una nafasi muhimu katika kuchangia usomekaji.

Kama Ngara, tunaunga mkono dhana kuwa usomekaji unajumuisha taratibu za kiisimu na yaliyomo katika matini, iwe chanzi au tafsiri. Ili kufikia usomaji unaodhihirisha mtazamo huo, msomaji wa matini tafsiri hana budi kuzingatia mambo kadha wa kadha katika matini husika. Haya ni pamoja na kuzingatia jinsi masharti na matarajio ya kiisimu, kisarufi, kisintaksia na kisemantiki yanavyotoshelezwa katika matini tafsiri inayosomwa. Hivyo hivyo, lazima aangalie mambo ambayo yanatawaliwa na sheria za lugha pokezi kama vile njeo na tahajia. Kwa upande mwingine mambo ambayo yanampa mtafsiri nafasi na uwezo wa kuteua, kwa mfano, kuteua msamiati ambao kwao ubinafsi na upekee wa mtafsiri hujitokeza. Pamoja na uteuzi wa msiamiati, mtindo wa mtafsiri katika kutekeleza tafsiri hautawaliwi na sheria fulani bali unahusiana sana na uteuzi wa mtafsiri. Aina hizi mbili za uteuzi ni vidokezi vinavyotumiwa na msomaji kujenga usomekaji au ufasiri badalia. Kwa hivyo, mtafsiri anapojenga mtindo sahili au hata mtindo changamano, upo uwezekano kwamba mambo mawili yatatokea. Kwa upande mmoja usomekaji rahisi na ufasiri wa moja kwa moja na kwa upande mwingine usomekaji tata. Hata hivyo, mambo haya yanaweza kurahisisha usomekaji au pia kuutatiza. Jambo la kimsingi hasa ni kwamba ili kuufikia usomekaji, mambo haya yote ni sharti yatiliwe maanani.

Tukichunguza mfumo mzima uliotumiwa katika *Madhabahu ya Kilio*, tunapata kuwa taratibu za lugha ya Kiswahili pamoja na msamiati uliotumiwa zinampa msomaji nafasi ya kuweza kutafsiri matukio yaliyomo bila matatizo. Katika *Madhabahu ya Kilio* Boge anaonyesha uzalendo wake kwa kutumia lugha inayoeleweka na inayosababisha ufasiri wa wazi. Anasema

> Huenda wanawake hawa walitaka kunitwanga kichwa kwa chupa za bia, lakini hawa bado ni dada zangu kwa hivyo, nakuomba usiwapige hawa picha wakiwa uchi wala wasichana wengine wowote wa nchi ya Kilima. (Uk 97)

Mambo haya anaambiwa Mzungu Silverspoon ambaye alikuwa akiwalewesha hawa wasichana wa Kilima wasiokuwa na kazi. Inaeleweka vyema kwamba mzungumzaji anaukashifu utamaduni wa kizungu wa wanawake kupigwa picha wakiwa uchi na hangependa mambo haya yasukumizwe kwa Waafrika. Haya pamoja na mengine mengi, yanatuonyesha kwamba watafsiri wametumia lugha inayouwezesha usomekaji rahisi na ufasiri wa moja kwa moja. Hivyo, katika sura hii tutajadili vepengee viwili muhimu vinavyoinua kiwango cha usomekaji wa matini. Kwanza, tutachunguza taratibu za kiisimu ambazo ni pamoja na upatanishi wa maneno na pili, tutachunguza muala wa mawazo unaochangiwa na taratibu hizo.

**2:2 Mwelekeo wa Kihadhira**

Usomekaji pia unachangiwa na mtazamo au uhusiano wa mwandishi/mtafsiri na msomaji. Ili kuhakikisha ukubalifu na utimilifu wa kazi inayotafsiriwa na hivyo kuhakikisha ubainikaji wa dhamira, mtafsiri hana budi kutilia maanani hali za kijamii, kitamaduni, kihistoria, kimatini na kifasihi zinazoizunguka kazi husika. Hali kadhalika hana budi kutilia maanani miingiliano ya kimatini inayodhihirika na jinsi inavyobainika katika kazi za kifasihi katika lugha pokezi. Sababu ya kimsingi ya kuyazingatia mambo haya inajikita katika ukweli kwamba kazi inayotafsiriwa inachangia lugha na fasihi pokezi kwa njia mbali mbali. Kwa hivyo, mtafsiri ni mwanasanaa; mwandishi anayezalisha na kuingiza katika fasihi na lugha pokezi mafunzo,

maadili na maarifa mapya. Kama ilivyo katika fasihi yoyote ile, tafsiri haifanywi pasina kutilia maanani hali halisi ambamo mtafsiri hujikuta. Ni sharti mtafsiri kama mwandishi ajinasibishe na maswala yanayomkumba katika hali yake halisi. Tafsiri ni sharti iende sambamba na mambo yatakayoifanya ijengeke kwa mujibu wa ukubalifu wake, mvuto pamoja na uhalisi utakaoifanya isomeke na kufasirika kwa manufaa ya hadhira pokezi. Hali hizi zinajidhihirisha katika *Madhabahu ya Kilio* kutegemea taratibu za kiisimu za lugha pokezi ambazo ni pamoja na upatanishi, urejelezi, udondoshi, usambamba na muala ambavyo vinafanya kazi pamoja ili kuinua kiwango cha matini.

**2:3 Taratibu za Kimatini**

Hatua ya mwanzo katika usomekaji mara zote inahusu jinsi masharti na matarajio ya kiisimu yanavyotoshelezwa. Hii ni kwa sababu usomekaji hauwezi kuwepo pasina kuwepo na uzingatiaji wa sheria za kiisimu katika hatua hii, mambo yote anayoyateua mtafsiri yanatawaliwa na sheria na hawezi kuenda kinyume na njeo, idadi, hali au hata mpangilio wa maneno.

**2:3:1 Upatanishi**

Upatanishi ni sifa ya kimatini, katika kiwango cha kiisimu ambayo huchangia mshikamano wa matini kiisimu. Sifa hii hutawaliwa na sheria za kiisimu na ni muhimu katika kuipa matini sura mahsusi. Kwa mujibu wa Beaugrande na Dressler (1981) na Neubert na Shreve (1992), mshikamano ni sifa ya kiisimu inayowezesha kushikanishwa kwa vipashio mbalimbali vya lugha. Kwa hivyo, mshikamano ni mbinu ya kiisimu inayojenga upatanisho wa kimawazo, kuunganishwa kwa dhana na hatimaye kujengeka kwa maana.

Mshikamano mara zote hauna budi kutawaliwa na sheria za lugha husika na sifa inayojitokeza katika kazi zote za kimaandishi ziwe zimetungwa asilia au zimetafsiriwa. Ni sifa ambayo ni sharti itimizwe hata kabla ya kuingia katika masuala ya uteuzi wa msamiati na mtindo. Kwa hivyo, usomekaji katika umbo la nje unawezeshwa na kule kutii sheria, masharti na matarajio ya kiisimu katika lugha husika. Kutii huku ni pamoja na kudumisha upatanisho wa ngeli, njeo, tahajia, miundo ya kisintaksia pamoja na kuafiki mifumo ya kisemantiki. Mfano huu kutoka *Madhabahu ya Kilio* unaonyesha hali hii ya utapatanisho wa kiisimu;

> Hedimasta aliingia katika baa, na huku akisimama kwenye kidato cha mwisho cha ngazi ya kuingilia, alichunguza kwa haraka mazingira hayo mapya. Aliingia kupitia kwenye ukuta wa kioo uliotenga baraza na sehemu nyingine ya baa akamwona Soita na marafiki zake, akawasalimu kwa kuwapungia mkono. Alikuwa na kimo kikubwa cha mwili. Mwingi wa madaha na daima alivaa tabasamu la kejeli. Akiwa mteja maarufu wa madhabahu ya kitaifa, hedimasta alijulikana kwa ukarimu wake, na jamaa fulani waliojifikiria kuwa wajanja, walikuwa wamezua mbinu za kujipatia pombe bure. (uk 8)

Nomino "Hedimasta", viambishi vya nafsi 'a' "mwingi wa madaha", "mteja", yote haya yanarejelea Hedimasta aliyeitwa mwanzoni mwa aya na kuleta ule

mshikamano wa vipengee vya lugha katika aya hiyo. Mshikamano huo unayahusisha mambo yanayozungumziwa kuhusu huyu Hedimasta hivi kwamba msomaji hana utata wa kufikiria katika sentensi fulani kuwa anayerejelewa ni mtu mwingine. Mfano mwingine ni huu;

> Gari moja lilipinda kushoto kwenye mzunguko na kuchukua barabara Ndovu na kuelekea alikokua Boge. Taa zake zilizowaka kwa nguvu zilimpofusha Boge kwa muda huku mwanga ukipenya na kuunda shimo gizani. Baada ya sekunde chache, gari hilo lilipunguza mwendo na kusimama. Lilikuwa limempita, lakini lilianza kurudi nyuma polepole kumwelekea Boge, huku taa zake ndogo za nyuma zikiwaka. (uk. 115)

Gari, linarejelewa kwa viambishi vya ngeli 'li' wakati inasemekana kuwa "taa zake zilimpofusha Boge" huku 'mwanga' ukipenya, msomaji anayapata kwa urahisi kuwa bila shaka 'taa' ni za gari vile vile 'mwanga' ni wa gari. Upatanishi huu unauondoa utata wowote ambao ungezuka kwa kufikiria kuwa taa ni za Boge au mwanga ni wa Boge. Hivyo upatanishi wa vipengele hivyo vya kiisimu huchangia pakubwa usomekaji wa kazi inayohusika.

Uthabiti wa matini hutegemea sana mshikamano wa karibu sana wa vipengele vya kisarufi vya kila namna. Mshikamano huu unaweza kuhusisha virai, vishazi, au sentensi. Asemavyo Beangrande, (1981).

> Uthabiti wa matini kama mfumo unashikiliwa na mwendelezo wa matukio (uk 48).
>
> (Tafsiri yetu)

Huu ni mwendelezo wa matukio mbalimbali katika matini. Kila tukio linatumiwa ili kuleta uelewa zaidi wa tukio lingine. Hivyo upatanishi huu wa kisintaksia unaweka utaratibu wa lugha katika matini.

Brow, G (1983), ana mtazamo huu. Akiunga mkuno mawazo ya Halliday na Hasan (1976) anashikilia kuwa kibainishi cha kimsingi cha kuonyesha kuwa sentensi hushikamanishwa pamoja ili kuunda matini ni upatanishi wa sentensi hizo zinazounda matini husika. Yaani, uthabiti wa matini yoyote ile unategemea uhusiano wa kiupatanishi wa vipengele vyake vya kiisimu. Uhusiano huu unaonyeshwa pale ambapo ufasiri wa kipengele kimoja katika matini unategemea ufasiri wa kingine. Kipengele kimoja kinazua utata wa kukifasiri ikiwa hakitawekwa katika muktadha wa kingine. Kwa Mfano, jambo moja muhimu linalopatikana katika matini na linaloiwezesha matini yenyewe kusomeka kwa urahisi na kwa mvuto mkubwa ni matumizi ya takriri au urudiaji wa maneno.

### 2:3:2 Urejelezi / urudiaji

Urejelezi ni mkakati wa matumizi lugha ambapo maumbo ya lugha ambayo yamekwishatumika katika sehemu zilizotangulia katika matini, yanatumiwa upya kwa njia mbalimbali zenye mahusiano kujenga mfumo mpya wenye maana, au unaopanua na kuendeleza maana. Urejelezi huweza kuwa, marudio ya moja kwa moja au usambamba.

### 2:3:3 Marudio ya moja kwa moja

Katika marudio ya moja kwa moja, vipengele vya kisintaksia kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, viwakilishi na kadhalika vinarudiwarudiwa. Urudiaji huu huweza kuhusisha virai, vishazi au hata sentensi moja. Kwa mfano, Osore na wenzake wanasema,

> Meneja aliendesha gari lake kasi zaidi ya kilomita mia moja kwa saa hadi ofisi yake binafsi iliyokuwa hatua chache tu kutoka kortini. Alimwita mhazili wake kwa simu akamtaka ampigie simu kwa mkuu wa sheria. Mkuu wa sheria aliduwaa alipoelezwa kuhusu hukumu iliyotolewa kwa washtakiwa hao. Mkuu wa sheria aliahidi kuchunguza kesi hiyo. Baadaye aliwaita watu wengine watatu na akatekeleza ahadi hiyo katika muda wa dakika kumi na tano. (uk 15)

Marudio ya maneno yaliyopigwa mstari yanamwezesha msomaji kubaini mara moja mhusika anayerejelewa. Pasipo kutumia marudio hayo, kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja'a' kingetumiwa. Lakini kiwakilishi hiki kingezua utata kwani katika masimulizi hayo mna wahusika watatu. Meneja, mhazili na Mkuu wa Sheria ambapo wote wanawakilishwa kwa kiambishi hicho 'a' cha nafsi ya tatu. Basi uamilifu wa marudio hapa ni kubainisha mhusika anayerejelewa na kuondoa utata ambao ungezuka, hivyo kurahisisha usomekaji. Marudio kama haya yanatokana na haja ya kuafiki na kutii sheria za kiisimu za lugha ya Kiswahili.Marudio haya kwa kiasi kikubwa hayashawishiwi na uteuzi wa msamiati.

Vile vile, marudio hutumiwa ili kusisitiza dhana au wazo fulani. Msisitizo huu humwezesha msomaji kuelewa zaidi yaliyomo katika matini au katika sehemuu ya matini. Hali kadhalika marudio haya, yanasaidia kujenga upeo na mwelekeo wa uelewa unaokusudiwa. Boge anapoingia na Kanaya mahali alimokuwa Billy Kanzika, anamuuliza hivi;

> Ninyi wawili mmewahi <u>kukutana</u>?
>
> La, sidhani <u>tumekutana</u>. <u>Tumekutana</u> kweli? (uk 17)

Kitenzi "kukutana" kimerudiwarudiwa ili kusisitiza kuwa watu hao hawajawahi kuonana. Ni dhahiri kwa msomaji kuwa, Boge na Billy Kanzika

hawajui ikiwa Billy na Kanaya wamewahi kukutana kwa vile wote wanauliza swali hilo. Uelewa wa msomaji unarahisishwa.

Mfano mwingine ni huu

> Nilisimama huku nikiwa nimekerwa sana, nikaweka mikono mifukoni mwa suruali yangu ndefu, nikaanza kutembea huku na huko, huku na huko, huku na huko, katika ukumbi huo mpaka mlango wa chumba kile ulipofunguliwa. (uk 49)

Maneno 'huku na huko' yamerudiwarudiwa ili kusisitiza kuwa msimulizi alikuwa amekerwa na alikuwa na wasiwasi mno ndiposa akawa anatembea juu chini, bila kutulia. Aidha, katika mfano wa kwanza kitenzi 'kukutana' kimesisitizwa.

Hali hii inadhihirisha upekee wa matini usiotegemea taratibu za kiisimu za lugha ya Kiingereza. Kwa mfano, mfano wa kwanza hapo juu unajitokeza kwa njia tofauti katika matini asilia. Katika *Shrine of Tears* Boge na Billy wanaulizana,

> Have you two met?
>
> No, I don't believe we have met. Have we? (uk 16)

Katika Kiswahili, sharti kitenzi 'kukutana' katika sehemu ya mwisho kiwepo ndiposa maana ikamilike. Lakini katika Kiingereza "Have we" inaonyesha hali hiyo ya kukutana. Taratibu za kiisimu za lugha hizi mbili ni

tofauti ndiposa inakuwa si haki kuihukumu matini tafsiri kwa mujibu wa sheria na kanuni za lugha asilia. Hili ndilo lengo la somo hili. Kuonyesha kiasi ambacho kazi tafsiri inaweza kusomwa bila kuifungamanisha na kazi asilia.

**2:3:4 Usambamba**

Usambamba ni ile hali ya kuzungumzia ishara ambazo tayari zimetumiwa lakini kwa kutumia vipashio tofauti-tofauti ili kujiepusha na marudio ya moja kwa moja. Marudio ya moja kwa moja yakitumiwa katika matini bila tahadhari huenda maelezo yakakosa maana. Katika *Madhabahu ya Kilio* ipo mifano ya usambamba kama;

> Alikuwa akitaka kuwapa glukosi wakati wa mapumziko, lakini sasa aliamua kuwapatia mara moja. Kwa hiyo, aliingia kile chumba akawamiminia waigizaji viganjani mwao sukari hii iliyotenda miujiza. Baadhi ya viganja hivyo vilikuwa vikitetemeka kwa woga. Waigizaji waliokuwa wachangamfu waliona shughuli hiyo ya Hedimasta kama ya kuchekesha na wakaanza kumwita, 'kocha mkuu-mgawaji wa nguvu. (uk 222)

Hapa dhana ya glukosi imeelezwa katika sentensi sambamba kwa maelezo tofauti tofauti – **sukari, nguvu** na **glukosi**. Ingawa vipashio ni tofauti,

vimetumiwa sambamba kuleta maana ile ile. Kwa njia hii msomaji anaepuka kule kuchoshwa kwa marudio ya vipashio vile vile.

Hali hii inajitokeza katika riwaya nzima kwa jinsi matukio mbalimbali yanavyotumiwa kisambamba kurejelea dhana moja. Kwa mfano, watafsiri wa *Madhabahu ya Kilio* walinuia kuonyesha wasomaji hali ya ukoloni mamboleo inayoendelea katika mataifa machanga baada ya kupata uhuru. Lakini dhana hiyo imewasilishwa kwa matukio mbalimbali kiusambamba. Kwa mfano, katika Madhabahu ya Kitaifa ya Kilima, shughuli za kitamaduni zinazoendelezwa pale ni za kizungu. Michezo inayoigizwa ni ya kizungu. Waafirika wanamhusudu Mzungu kuliko mwafrika mwenzao kama inavyoonekana katika hoteli ya Silver Spoon. Waafrika wanaamini kuwa elimu humu barani Afrika ni duni ndiyo maana wanakwenda ng'ambo kusomea huko. Kwa mfano, Vanity na Kamonya hawakupata digrii zao humu. Matukio haya yote na mengine mengi yanaashiria jambo moja. Kuwa Waafrika walifanywa kuamini kuwa kila kitu chao ni duni. Hivyo nyenzo za kizungu sharti ziendelezwe. Hali hii inarahisisha ufasiri wa lengo kuu la watafsiri na uamilifu wa matini hii kwa upande wa fasihi na dhima yake.

**2:3:5 Viwakilishi**

Viwakilishi ni njia ya mkato ya kutumia nomino ili kujenga mshikamano wa kiisimu katika tungo. Viwakilishi vinatumika kuwakilisha na kuwasilisha nomino za aina mbalimbali. Hii ni njia inayowasilisha mambo kwa mkato, inayoepusha marudio ya mara kwa mara ya maelezo marefu na ni njia inayotawaliwa na sheria za kiisimu za lugha maalum. Kwa mfano katika *Madhabahu ya Kilio,* viwakilishi vyote vinatawaliwa na sheria za kiisimu za lugha ya Kiswahili.

Kwa mfano;

> Wakati mmoja, Boge alijikuta amesimama kwenye mlango wa hoteli mpya. Namna alivyosimama ilionekana kana kwamba alitaka kuingia ndani lakini alikuwa akizuiliwa na mkono wa mtu ulioshika kwa nguvu sehemu ya nyuma ya shati lake. (uk 77)

Kiambishi 'a' kimetumiwa kuleta ule upatanishi wa ngeli ambao unamwonyesha msomaji uhusiano uliopo baina ya matukio yanayozungumziwa na mhusika Boge. Kimetumiwa badala ya kurudiarudia jina Boge kila mara. Urudiaji wa mara kwa mara ni jambo ambalo huepukwa katika lugha nyingi, lugha ya Kiswahili ikiwemo. Uepukaji huo ni njia ya kuzuia ukariri, uchoshi na uelezaji mambo kwa mzunguko. Hii ndiyo mbinu inayoitwa 'anafora' katika isimu ambapo kiwakilishi kinatumiwa baada ya jina linalowakilishwa. Mbinu hii hutumiwa sana kwa sababu inamwezesha

msomaji kutambua mwanzoni kabisa kitu kinachorejelewa halafu anapokumbana na viwakilishi vya kitu hicho anavihusisha nacho.

Vile vile, ipo mbinu ya 'katafora' ambayo hutumiwa. Katika mbinu hii, virejeshi hutumiwa kabla ya kinachorejelewa. Kwa mfano, kirejeshi kinaweza kutangulia kabla ya mhusika kutajwa.

> Akiwa na wasiwasi huu akilini mwake, Boge alisimama mara moja na kuchungulia kwenye giza lililomzunguka na lile lililotanda huko mbele ya kidimbwi. (uk 76)

Mara nyingi mbinu hii ikitumiwa husaidia kuleta hali ya taharuki ya muda mfupi ambapo msomaji anapatwa na hamu ya kutaka kuendelea ili kugundua kinachorejelewa. Kwa mfano,

> Hatimaye mvua ilipopusa, na waombolezaji wakawa wanajitayarisha kurudi makwao, yowe la mwanamke lilipasua hewa nyevu ya alasiri. Punde yowe jingine likapigwa na jingine pia. Hapo awali watu walidhani mmoja wa jamaa ya Kanaya alikuwa amefika kushuhudia mazishi ya Kanaya, akakuta mazishi yamekwisha lakini walikosea kwa kuwa kilio kilisambaa kuzunguka mji wa Michael Luta.
>
> Nyanya alikuwa amekufa. (uk 161)

Aya nzima inazua hali ya taharuki japo kwa muda mfupi ya kutojua chanzo na sababu ya kilio kilichosikika kwa ghafla. Hali hii inampa hamu msomaji ambaye anataka kujua kilichojiri, na hatimaye kilichokuwa kikirejelewa au kikizua hali ya taharuki kinatajwa: "Nyanya alikuwa amekufa".

Hali ya uwakilishi inajitokeza katika matini nzima.Mwanzoni mwa matini Boge ameelezwa kama mhusika anayejiuliza maswali mengi ya kushangaza wengine. Kwa mfano,

> Kwa hivyo huendelea kuuliza maswali. Maswali ambayo huzidisha shinikizo zisizohitajika kwenye matatizo makubwa ya taifa la Kilima. Maswali makali yenye pande mbili, maswali ya ndumakuwili; ambayo majibu yake yanapotolewa bila hadhari huonekana upuzi mtupu….
> (uk 161).

Maswali haya yanawasilisha hoja nzito kabisa tunazokumbana nazo katika matini mzima. Boge ana shaka na hali ya utamaduni wa Mwafrika kutotiliwa maanani, hali ya elimu katika kilima, uwajibikaji wa viongozi, matumizi ya mali ya umma na kadhalika. Hivyo maswali yaliyo katika ukurasi wa mwanzo kabisa, yanazua hali ya taharuki lakini hali halisi au chanzo cha maswali hayo kinajitokeza katika matini nzima.Taharuki ni mbinu

muhimu ya uandishi katika fasihi ya Kiswahili na ambayo inachangia usomekaji wa kazi husika.

### 2:3:6 Udondoshaji wa maneno

Udondoshaji ni mbinu ya uandishi au uzungumzi ambapo vipashio fulani vya kiisimu huondolewa ili kufupisha maelezo. Hii haina maana kuwa hoja nzito hupuuzwa. La! Vipashio fulani fulani vinadondoshwa katika matini ili kuepukana na urudiaji usiofaa. Kwa msomaji wa matini husika, sharti uelewa kuwa ana umilisi mwafaka wa lugha husika uwepo. Udondoshaji huu aghalabu hutokea katika tungo tofauti zinazohusiana. Hata hivyo sharti pawe na uhusiano wa karibu sana baina ya kipashio kinachodondoshwa na kile kinachorejelewa. Mara nyingi vitenzi ndivyo hudondoshwa ingawa kuna uwezekano wa udondoshi huo kutokea pale ambapo nomino zinahusika. Kwa mfano katika *Madhabahu ya Kilio,*

> Madhabahu ya kitaifa ya Kilima yamezingirwa na asasi mbalimbali: Jumba la kitaifa la kutangazia kwenye upande wa kaskazini, chuo kikuu cha kitaifa kwenye upande wa magharibi, na hoteli kubwa ya kimataifa ya 'Five Star' upande wa mashariki. (uk 2).

Kitenzi 'kuzingirwa' kimedondoshwa katika sentensi au katika vipashio vinavyofuata lakini dhana ya kuzingirwa imejitokeza kwa kuvifasiri vishazi hivi kwa muktadha wa kishazi cha kwanza. Mbinu hii huchangia usomekaji hivi kwamba maandishi yanakuwa mafupi yasiyomchosha msomaji. Kwa mfano,

> Ndoto hii imenijia mara mbili mwezi mmoja. Mara, ya kwanza ilikuwa tarehe tisa na ya pili tarehe kumi na tatu. (uk 19)

Mbinu hii inapotumiwa na mtafsiri, huwa inachangia mfumo wa taratibu za kiisimu za lugha pokezi. Husaidia kuiunda matini ambayo ina mshikamano mwafaka na madhubuti. Huu ndio mtazamo wa Beaugrande, R (1981) anapodai;

> Mbinu nyingine ya upatanisho inayochangia uthabiti na ustadi wa matini ni udondoshi. (uk 66)
> (Tafsiri yetu).

Jambo linalojitokeza hapa ni kuwa uthabiti na ustadi huu unapimwa kwa mujibu wa msomaji. Kwamba hadhira pokezi ndiyo hushawishi udondoshi ili iweze kusoma kazi inayoafiki matarajio yao. Mambo haya ya uthabiti na ustadi wa matini huchangia katika kuinua kiwango cha usomekaji. Matini thabiti mara nyingi huweza kusomeka na kufasirika na msomaji na huo ndio uhusiano uliopo baina ya udondoshaji na suala zima la usomekaji. Usomekaji kwa kiasi kikubwa unachangiwa na huu uwezo wa kusoma kwa hadhira lengwa ambapo haijalishi ikiwa ni matini asilia au tafsiri. Haijalishi

kwa sababu mwandishi wa matini asilia na mtafsiri wote ni wasanii walio na nafasi mahsusi katika jamii wanamoandikia. Gilliland, J (1972) anaposhughulikia usomekaji anawanukuu Dale na Chall (1948) waliposema;

> Kwa upana, usomekaji ni jumla (yakiwemo maingiliano) ya vipengee vyote katika maandishi vinavyopelekea kufaulu kwa usomaji. Kufaulu kunajumuisha kiasi cha uelewa wa matini, uwezo wa kusoma kwa ufasaha na jinsi inavyovutia. (Uk 12-13)

Udondoshi unashawishiwa na haja ya matini kusomeka kwa ufasaha na kwa urahisi kwa upande wa wapokezi. Hoja hii inalenga hadhira pokezi inayotarajiwa kufurahia kazi yenye mshikamano unaofaa. Kwa mfano

> Boge ni mwotaji ndoto, tena ni mgonjwa. (uk. 1)

> Dora aliingia ndani na kufunga mlango (uk. 210)

> Dora alipomkaribia Kamonya aliinyosha mikono yake na kumkumbatia mara kadhaa.... (uk 226)

Badala ya kurudiarudia nomino husika au kutumia viwakilishi vyake, nomino hizo zimedondoshwa. Lakini kwa msomaji, matukio yamesawiri uhusiano hivi kwamba hata bila nomino kurudiwa, inabainika kuwa zinahusika kwa mfano katika “Boge ni mwotaji ndoto, tena ni mgonjwa”. Inabainika wazi kuwa yule yule Boge ambaye ni mwotaji ndoto ndiye mgonjwa. Vile vile katika “Dora aliingia ndani na kufunga mlango”, hajatajwa kuwa ndiye Dora akafunga mlango bali ni wazi kuwa alipoingia

ndani, alifunga mlango. "Dora alipomkaribia Kamonya aliinyosha mikono yake na kumkumbatia mara kadhaa." Uhusiano wa upatanisho unaoletwa na kiambishi 'm' katika kumkumbatia unatuonyesha kuwa Kamonya ndiye aliyekumbatiwa ingawa hajatajwa tena katika kishazi cha mwisho.

### 2:3:7 Njeo na hali

Kuna njia za kutambua njeo na hali katika matini. Nyakati huonyeshwa katika vitenzi vinavyotumiwa. Lugha ya Kishwahili ina njeo tatu muhimu na hali mbalimbali zinazoambatana nazo. Wakati uliopo unaowakilishwa na kiambishi –'a'-, wakati uliopita 'li' na wakati ujao 'ta'. Hali ya kuendelea huwakilishwa na kiambishi 'na' na hali timilifu huwakilishwa na 'me'-. Viwakilishi hivi hujidhihirisha katika matini kulingana na matukio yalivyopangwa. Katika *Madhabahu ya Kilio* tunaona matumizi ya njeo hizi ambapo njeo ya wakati uliopita imetawala. Wakati huu unaoanisha matukio katika matini na kuyapa muumano wa pamoja unaomwezesha msomaji kuhusisha tukio moja na lingine kwa urahisi kwa jinsi matukio hayo yalivyofuatana. Mfano ufuatao unaonyesha uhusiano wa matukio yanayoelezwa kulingana na jinsi yalivyotukia kwa mfuatano.

> Punde si punde a<u>li</u>kuwa mikononi mwetu. A<u>li</u>kuwa a<u>ki</u>kwaruza na kurarua chochote a<u>li</u>chokigusa. Kwa muda wa sekunde

chache alikuwa amebadilisha shati la Boge kuwa mararuraru na kuanza kukipiga ngumi kifua cha Boge kilichoachwa wazi. (uk 47)

Tunaona kuwa matumizi ya –'likuwa' na –'ki' katika 'alikuwa akikwaruza' yanaonyesha kuwa alikuwa akiendelea kutenda kitendo hicho halafu tunaambiwa kuwa, 'kwa muda wa sekunde chache alikuwa tayari ametimiza kitendo cha kulifanya shati la Boge kuwa mararuraru na akaanza kukipiga kifua chake. Matumizi ya viwakilishi hivyo vya nyakati yameyaoanisha matukio kiasi cha msomaji kuweza kuyafuata kwa makini bila kukanganyikiwa. Hali hii inabainika Kamonya anapong'ang'ania kuwahakikishia kuwa ipo sera ya utamaduni nchini Kilima. Anasema;

> Kabla sijaenda India niliona hati rasmi ya sera ya Utamdauni ya Kilima katika maktaba ya shule ya sheria. (Uk 29)

Viambishi vya nyakati vilivyotumiwa vinaonyesha kuwa hati ya sera ya utamaduni ilionekana zamani. Kabla, –ja na –li yanasawiri uhalisi huu kwamba wakati Kamonya alikuwa humu nchini kabla ya kwenda India, aliiona hati. Ni baada ya Kamonya kuyatamka maneno hayo ndipo msimulizi anagundua kuwa alikuwa mwanafunzi huko India na alikuwa amekuja kwa likizo. Anasema,

> Nilikuja kugundua baadaye kwamba Kamonya alikuwa mwanafunzi wa shahada ya pili katika chuo kimoja huko India. (uk 29).

Msomaji wa matini hii anaweza kuelewa kwa urahisi mfuatano wa matukio kwa jinsi viambishi vya njeo vimetumiwa ili kuoanisha matukio mbalimbali katika matini hata bila kuwa na ufahamu wa matini chanzi. Hata hivyo, msomaji ambaye labda ameisoma matini chanzi anaweza kutatizwa pale ambapo anakumbana na taratibu zinazojaribu kulazimisha uelewa asilia juu ya matini pokezi. Kwa mfano, katika baa ya Hells Gate tunaambiwa katika matini asilia hivi baada ya Boge kuagiza kinywaji chake;

> The woman did not move. Instead she just stood there gaping at him. Finally when she was sure that he was a beginner she offered him a little education. "Money Mbrantha, here we pay as we ndrink." (uk 76)

Tafsiri yake katika *Madhabahu ya Kilio*

> Mwanamke huyu hakubanduka; badala yake alisimama pale akimtazama Boge. Hatimaye, alipoona kuwa Boge alikuwa mwanagenzi aliamua kumwelezea hali ya mambo ilivyo. (uk 79)

Tunaona kuwa watafsiri wa *Madhabahu ya Kilio* wametumia hali inayoweza kumtatiza msomaji katika makala pokezi. Msimulizi anasema, "she offered him a little education". Tena, kwa usemi halisi anamwambia ampe pesa ili ajue kuwa hapa ni pesa kwanza halafu bia baadaye. Lakini katika kutafsiri, usemi huu halisi wa kuonyesha kuwa mhudumu huyu alitaka pesa haupo. Badala yake wanasema tu kuwa, "… aliamua kumwelezea hali ya mambo ilivyo." Neno "ilivyo" nalo linaashiria wakati gani? Bila shaka ni wakati uliopo ambapo masimulizi haya yalikuwa tu ya matukio ya zamani. Hali ya awali katika matini asilia (mhudumu kutaka pesa) imepuuzwa. Haya

yote yanamkanganya msomaji na kuutatiza uelewa wa kauli hiyo hivyo kuathiri usomekaji.

## 2:3:8 Viunganishi

Viunganishi ni vipashio muhimu katika lugha vinavyotumiwa kuunganisha tungo mbili ili kuleta mshikamano wa matukio ambapo mshikamano huo hujenga muala na kuwezesha tungo kueleweka kisemantiki. Kuna viunganishi vinavyounga matukio yanayotegemeana katika sentensi kwa mfano;

> Boge aliingiza mkono wake kwenye mkoba wa ngozi na kutoa kidaftari. (uk 19)
>
> Sikuamini yale niliyokuwa nikisikia kutoka kwa Jay Boge. Nilitaka kupasua kicheko niucheke mzaha huu wote, lakini nilikumbuka alivyoudhika Soita alipotaja jambo hilo kimzaha (uk 19).

Kiunganishi 'na' kimetupa taarifa kuwa Boge hakufanya kitendo cha kuingiza mkono tu bali pia alitoa kidaftari. Kiunganishi 'lakini' kimetumiwa kuonyesha utegemezi wa mambo mawili. Mzungumzaji alitaka kupasua kicheko. Kilichomzuia ni kukumbuka jinsi Soita alivyoudhika. Msomaji anayaoanisha matukio haya kwa kuyahusisha akitumia kiunganishi –'lakini'.

Matumizi haya ya viunganishi yanajitokeza hata kwa matukio yaliyomo kitabuni. Kwa mfano, katika sherehe za mazishi ya Kanaya matukio kadhaa yameunganishwa ili kutufunulia ukweli wa mambo katika Kilima. Kuna mgogoro kati ya babake Kanaya na wazee wa ukoo kuhusu mahali atakapozikwa Kanaya. Tunaonyeshwa jinsi utamaduni wa ukoo wa Kanaya bado umekita mizizi miongoni mwa wazee vijijini. Hapo hapo, tunapata kuwa mazishi yanacheleweshwa kwa vile wapiga picha wa Mhe Mbagaya hawajawasili. Mvua kubwa imenyesha hivyo wapiga picha hao wanachelewa njiani. Matukio haya yana uhusiano kwa vile, huyu mheshimiwa Mbagaya ndiye mbunge wa sehemu hiyo bali hajajishughulisha na ujenzi wa barabara. Nao uunganisho huo ulinuia kutueleza kuwa viongozi waliopewa mamlaka ya kuhudumia wananchi baada ya uhuru hawakuzingatia kazi zao kwa makini.

Viunganishi vimetumiwa ili kuleta uamilifu wa matini hii kuwa, inaangazia upatanishi wa vipengee vya kiisimu vinavyofungamana na lugha ya Kiswahili. Upatanishi huu unaiwezesha kazi hii kusomeka katika lugha ya hadhira lengwa hata isipoangaliwa kwa misingi ya matini asilia. Huu ndio mwelekeo wa kulichunguza somo la tafsiri ambao unaegemezwa kwa mtafsiri na si mwandishi wa matini asilia. Uchunguzi wa namna hii unaipa tafsiri nafasi ya kujisimamia kama matini yenye mshikamano wenye upekee wake kwa mujibu wa lugha pokezi.

Hali hii inaweza kulinganishwa na hali ya mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni kujaribu kujisimamia baada ya kupata uhuru. Hali ya mataifa haya kutaka kujiondoa katika minyororo ya nyenzo za kikoloni zilizoziweka hali zao chini. Hivyo hivyo kupitia kwa tafsiri, lugha zilizodaiwa kuwa duni na ndogo zinajaribu kuinuliwa na kutambulika. Kimsingi, hizi ndizo baadhi ya taratibu au kaida za kimatini zinazoiwezesha kazi kusomeka hasa zinapompa msomaji nafasi ya kuibua usomaji na ufasiri unaoafikiana na matarajio yake

katika lugha na fasihi pokezi. Matarajio kwamba katika lugha, zipo taratibu za kiisimu ambazo hufuatwa ili kuunda matini yenye uthabiti.

## 2:4 MUALA

Muala ni mfuatano wa matukio kwa utaratibu kiasi kwamba yanakuwa na mshikamano wa mawazo katika matini nzima. Hivi ni kusema kuwa, matini huleta maana kwa sababu ina mfululizo wa matukio ambayo hutegemeana yakiwa katika sentensi zinazofuatana ili kuleta maana. Mfululizo huu wa matukio yenye maana zinazohusiana ndio msingi wa muala katika matini.

Sentensi zinavyofuatana ni njia moja ya kuonyesha muala. Muala pia unaweza kubainika nje ya mipaka ya sentensi. Ishara zinazotumiwa katika matini ili kusawiri maana fulani hujengeka katika misingi ya dhana na huweza kufasiriwa na msomaji kwa kuzingatia uhusiano wa dhana moja na nyingine hata kama hazipo katika mahusiano jirani katika sentensi lakini mradi ishara hizo zimo katika matini. Hivyo, usomekaji wa kazi yoyote ile unachangiwa na vipengee vilivyoundwa kwa mshikamano wa mawazo yenye uhusiano wa aina fulani, yawe katika ujirani wa karibu karibu au yawe yamesambazwa katika sehemu mbali mbali za matini.

Hii ndio maana inayojitokeza David Birch (1981:20) anaposema kuwa muala katika matini ni dhana inayohusu uhusiano wa yale yanayosemwa na hali halisi ya maisha ya binadamu. Hoja hii ina maana kuwa msomaji anaposoma matini fulani, anapata kuwa mambo anayoyasoma ni ambayo yanawezekana katika ulimwengu halisi na kwa hivyo anayaelewa kwa kuwa yanajinasibisha na mahitaji yake. Aghalabu mambo haya huwa yamepangwa kwa utaratibu unaoyawezesha kueleweka na kufasirika. Kwa misingi ya tafsiri muala unatokana na jinsi mtafsiri anavyotumia lugha pokezi kupanga na kusawiri ujumbe unaoafikiana na matakwa na matarajio ya msomaji wake.

Mtaalam mwingine kama vile Dijk T.A.V ameweza kulitafiti swala hili la muala katika matini za aina mbali mbali na kuibuka na taratibu zinazochangia mshikamano wa dhana. Anasema kuwa muala unahusu jinsi mawazo fulani yanavyopangwa katika matini na kujenga uhusiano mwafaka wa mahusiano ya dhana. Dhana hizi kimsingi, zinakuwa na ukweli fulani wa kimahusiano. Mpangilio wa sentensi unaingiliana na mpangilio wa mawazo. Katika *Madhabahu ya Kilio*, mfano huu unaeleza hali hiyo.

> Mwanamke mmoja ajuza aliyefikiria kuwa huenda pasiwe na nafasi ya kutosha mle nyumbani kwa watu wote ambao wangependa kulala, tayari alikuwa ameingia mvunguni mwa

meza akaitandika kanga yake na sasa alikuwa amelala usingizi mnono. (uk. 100)

Je, kifungu hiki kina muala? Kwanza, kuna kiima 'mwanamke' kisha, kuna kiwakilishi 'a' kinachohusishwa au kumrejelea mwanamke huyo. Tukiendelea, tunapata dhana ya kulala na kifaa ambacho ni kanga ambavyo vinahusiana na huyu mwanamke. Kwa upande mwingine tuna 'nyumba' na vitu vinavyohusiana nayo. Watu wanaweza kupatikana katika nyumba. Pia meza ni kifaa kipatikanacho katika nyumba. Kwa kuwa kuna uhusuiano wa aina hiyo, tunasema kuwa kifungu kina muala. Vile vile viarifu vilivyotumiwa vinaonyesha muala kwa jinsi vinavyohusisha matukio katika kifungu chenyewe. 'Mwanamke" na 'nyumba' vinahusiana tukizingatia vitenzi vinavyohusika. Kwa mfano, mwanamke <u>alifikiria</u> kuwa kungekosekana nafasi ya kutosha watu wote kulala. Hii ndiyo sababu alikuwa tayari ameingia mle nyumbani na kutandika kanga yake mvunguni mwa meza na kulala. Kuna uwiano mkubwa baina ya matukio hayo. Ikisemekana tu kuwa 'alitandika' kanga mvunguni mwa meza na kulala, ingawa ni sentensi sahihi kisarufi, maana yake haitakamilika bila sentensi ya mwanzo kuwa alifikiria kuwa hapana nafasi ya kutosha watu wote. Hivyo muala ulio hapa unampa msomaji nafasi ya kuyaelewa matukio na visababishi vyake pamoja na matokeo yake.

Kwa mujibu wa maelezo haya, muala ni jambo la kimsingi katika usomekaji. Hii ina maana kwamba mbali na kuafiki masharti ya kiisimu, hatua ya pili ya usomekaji inajitokeza katika daraja ya muala kwamba masharti ya kiisimu yanawezesha kubainika kwa mshikamano wa mawazo, matukio pamoja na kudhihirika kwa matukio. *Madhabahu ya Kilio* ni kazi ambayo ina muala unaoeleweka tangu mwanzo hadi mwisho kwa kuwa msomaji anaweza kuona mshikamano wa mawazo pamoja na mfululizo wa matukio. Kuna muala katika daraja ya sentensi na pia katika daraja ya matini nzima.

Uelewa wa matini hutegemea miundo ya kisintaksia na leksia za maneno ili kufikia ufasiri wa aina yo yote ile (Brown, G 1984). Yaani, tunaweza kutambua tungo fulani ambazo ni sahihi kisintaksia bali ambazo haziwezi kufasirika kimaana kwa sababu tunahitaji maelezo zaidi. Hadi maelezo hayo yawepo ndipo muala unapatikana katika matini. Kwa mfano, katika *Madhahahu ya Kilio*;

> Teksi moja nadhifu mithili ya gari la kubebea maiti la London ilikata kona kushoto ikaacha barabara ya Churchill ikaja polepole mpaka mahali tulipokuwa. Gari hili liliegeshwa mkabala na lango kuu la hoteli. Milango yake ilifunguliwa mithili ya

> kunguru afunguapo mabawa yake na dereva akatoka nje. Alipotutazama alifahamu mara moja kwamba ni sisi alikuwa ametumwa kuchukua. (uk 51)

Maelezo haya yanamhimiza msomaji kuendelea kusoma ili kutambua jambo hasa linaloashiriwa na sentensi tangulizi. Mwanzoni, kifungu kinaeleza jinsi teksi ilivyo, kisha jinsi ilivyokuja. Bila sentensi ya mwisho inayoeleza kilichotukia baada ya teksi aina hiyo kuja kwa mwendo unaozungumziwa, sentensi za mwanzo haziwezi kuleta maana kamili. Basi kwa kukamilisha kuwa dereva huyo alitambua ni wao aliokuwa ametumwa kuwachukua, msomaji anapata kukamilisha hamu yake ya muda mfupi na kuingiwa na hamu zaidi ya kutaka kujua alichofanya dereva baada ya kutambua kuwa wale ndio watu aliokuwa ametumwa kuwachukua.

Aya inayofuata inajazia hamu hii kwamba;

> Kamonya alikuwa wa kwanza kuingia huku akisindikizwa na yule mwanamke mzungu aliyekuwa akimhudumia ...... (uk 51)

Dereva alipotambua kuwa ni wao aliofaa kuwachukua, kilichofuata ni kuwa walianza kuingia garini. Hapa kuna muala kwa jinsi kuna mwendelezo wa matukio yaliyo na uhusiano.

Muala unaojitokeza katika kiwango cha sintaksia huwa ni daraja ya kutuelekeza mfululizo wa matukio yanayounda matini nzima. Kadiri matukio yanavyohusiana na kuchangiana katika kuendeleza ploti na kuridhia malengo ya mtafsiri, ndivyo usomekaji wa kazi husika huweza kuafikiwa. Katika *Madhabahu ya Kilio*, uhalisi huu umejitokeza hivi kwamba matini inaweza kusomeka na kufasiriwa kwa upekee wake bila kufungamanishwa na matini asilia. Maelezo yafuatayo yataonyesha hali hii.

Boge ni kijana ambaye ana maswali mengi kiasi kwamba Wakilima wenzake wanashindwa kumwelewa. Lakini tunapoendelea kusoma, tunabainikiwa na ukweli kuwa Boge ni kijana ambaye haelewi hali inayomzunguka katika nchi ya Kilima kwa sababu anayaona mambo katika uhalisia tofauti na Wakilima wengine. Anawakilisha vijana wasomi ambao wamezinduka na kuweza kuyaona matatizo yanayoikumba nchi yao. Maswali anayojiuliza bila kupata majibu yanatokana na hali ilivyo katika nchi ya Kilima baada ya ukoloni. Haelewi vipi Wakilima wanauhusudu utamaduni wa mzungu na kuudunisha wao wenyewe, ubadhirifu wa kutumia mali ya umma vibaya, na wananchi kuwahusudu viongozi na kadhalika. Hata hivyo, anapojiuliza maswali haya, anaelewa vyema kwamba hali inayochochea haya yote ni uwezo wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, na wa kielimu ambao unadhibitiwa na wazungu na sio Waafrika. Kuhusu sera ya utamaduni, anawashauri wenzake;

> Tunachohitaji kwa dharura ni sera kamili ya utamaduni na WaKilima wachanga wenye ujuzi na waliojitolea kuitelekekeleza kikamilifu sera hiyo hadi mwisho. (uk 29)

Ushauri huu ni dhihirisho kuwa Boge anaelewa chanzo cha hali inayoikumba Kilima na jinsi Wakilima wanavyoweza kuweka bidii

kubadilisha hali yao ya maisha kuhusu elimu. Mazungumzo kati ya Boge na Vanity yanaelekea kuonyesha kuwa elimu ambayo Wakilima walipewa haithaminiwi. Boge anashangaa vipi Vanity alivyoweza kuhitimu na kupata shahada ya Ph.D haraka vile. Na aliporudi kutoka Marekani akiwa na shahada hiyo, aliteuliwa mara moja kuwa mhadhiri katika mojawapo ya idara katika kitivo cha Elimu. Haya ndiyo baadhi ya mambo yanayochochea maswali mengi akilini mwa Boge, hali ambayo inaonyesha muala ulio katika matini nzima. Matukio yameweza kuelezwa huku visababishi vyake vikionyeshwa. Hali hii inarahisisha usomekaji kwa misingi ya ufasiri unaowezeshwa kupitia kwa muala uliomo. Yaani ule mshikamano wa mawazo katika matini nzima.

Pia, katika safari ya kwenda Seboa kwa mazishi ya Kanaya, magari yanakwama kwa vile barabara zina matope mengi kutokana na mvua nyingi iliyonyesha. Ukweli ni kuwa viongozi wanaosimamia idara mbalimbali katika serikali wamepuuza kazi zao kama vile Mhe. Mbagaya ambaye ndiye Mbunge wa eneo hilo alivyopuuza barabara hizo. Anapoambiwa kuwa wapiga picha walizuiwa kufika pale kwa wakati uliofaa kwa sababu barabara haipitiki, anakuwa mkali sana ili kuficha uovu ulioko serikalini. Tunaona muala hapa kwa jinsi kuna muoano mkubwa baina ya matukio hayo. Hali hii ya muala imeweza kubainika katika matini nzima huku ikijinasibisha na malengo ya utafiti huu ya kuchunguza usomekaji kwa maana ya ufasiri na taratibu za kiisimu kwa jumla. Muala huu unategemea mambo mawili muhimu. Kwa upande mmoja, kuna maarifa waliyo nayo wasomaji juu ya hali halisi za maisha na kwa upande mwingine, jinsi malengo ya wahusika yanavyojitokeza katika matini.

### 2:4:1 Hali halisi ya maisha

Muala katika matini pia huchangiwa na uhusiano baina ya matukio katika matini na maarifa tuliyo nayo ya hali halisi ya maisha ya ulimwengu. Hii ina maana kwamba zipo nyakati ambapo muala ni jambo lililo nje ya mipaka ya sentensi na mtini. Kinachojitokeza hapa ni kwamba muala ulio nje ya matini ni kiungo kinachounganisha uhalisi wa matini na uhalisi wa hali ya maisha. Ukweli wa kile kinachotendeka ndani ya matini mara nyingi hauachani na kile kinachotokea katika maisha halisi. Hii ndio maana kuaminika kwa matukio ya kimatini kunategemea kuaminika kwa matukio hayo katika hali halisi ya ulimwengu. Beaugrande (1981) analitambua jambo hili anapodai;

> Swala la jinsi watu wanavyojua kinachoendelea katika matini ni zao mahsusi la swala la jinsi watu wanavyojua kinachoendelea katika ulimwengu (uk 30). (Tafsiri yetu)

Yaani, ufasiri wa matukio katika matini unategemea mambo ambayo wasomaji wamewahi kuyashuhudia katika maisha. Mwandishi si lazima aeleze kila kitu kuhusiana na ishara anazozitumia. Inajulikana kuwa msomaji ana umilisi wa mambo hayo. Kwa mfano, mwandishi anapoeleza kuhusu hospitali, inaaminika kuwa msomaji anafahamu kuwa hospitalini mna daktari,

madawa, wagonjwa, machela na mambo mengi mengine yanayohusiana na utabibu. Katika *Madhahabu ya Kilio;*

> Boge, ambaye bila shaka alitaka kuwa pekee yake, alichagua meza iliyokuwa pembeni kabisa, akaketi. Mhudumu wa kike aliyekuwa akisinzia karibu na sanduku la santuri lililoharibika aliamka kutoka usingizini na kuinuka. Alifurahia kupata mteja katika mojawapo ya meza alizokuwa ametengewa kuhudumia jioni hiyo. Aliinua mkono wake juu akapiga miayo, kisha akatembea polepole kuelekea kwenye kaunta (uk 78).

Hata bila kuambiwa, vitu kama 'meza', 'mhudumu' 'sanduku la santuri' 'mteja' na 'kaunta' ni vitu vinavyonasibishwa na baa au mkahawa. Hata mwandishi asipotaja mahali penyewe yaani mandhari, tayari yanamwelekeza msomaji na kufanya usomekaji wa matini hii kuwezeshwa. Wataalam kama Beaugrande na Dresster (1981) wanasema kuwa umilisi huu wa binadamu ni picha za akilini.

> Umilisi uliomo akilini mwa binadamu hueleza vitu vinavyokwenda pamoja wala sio jinsi vinavyokwenda pamoja au jinsi vinavyofuatana (uk 90).

Anamaanisha kuwa vitu hivyo viko katika umilisi wa binadamu na hata bila kuvitaja inajulikana kuwa vipo. Hali hii imejitokeza katika matini nzima kwa jinsi mandhari, vifaa na dhana zilizowasilishwa zinaoana na hali halisi. Katika

ulimwengu wa msomaji. Hii ndiyo sababu inayoipa matini hii utimilifu na uamilifu kwa mujibu wa fasihi ya Kiswahili kwani fasihi aghalabu husawiri hali halisi ya maisha ya binadamu.

### 2:4:2 Lengo la mhusika

Muala pia huonyeshwa kwa jinsi mhusika mmoja anavyosawiriwa kuanzia mwanzo hadi mwisho akiwa na lengo au malengo maalum aliotengewa kuyatimiza. Katika hali hii msomaji anafuatilia mfululizo na mzunguko wa matukio na kasha kushuhudia yanavyotelekezwa, jinsi yanavyohusishwa na jinsi yanavyoendelezwa. Muundaji wa matini ya aina hii hupanga visa, matukio pamoja na mambo yote yanayohusiana na mhusika huyu kulingana na jinsi mwandishi alivyodhamiria. Kwa mfano, matukio yote yanayomzunguka mhusika Dora katika riwaya ya *Madhabahu ya Kilio* yana lengo, yanafuata mpito wa wakati kimantiki na yanahusiana kwa njia inayoaminika. Lengo lenyewe ni kujenga uhusiano wa karibu sana na Jay Boge, mwanasanaa mashuhuri. Tunapokutana naye kwa mara ya kwanza, ni katika mahali palipotokea ajali iliyopelekea kufa kwa Kanaya. Msimulizi anatusawiria Dora kwa mnato kabisa kuanzia hapa;

> Mwanamke wa umri wa makamo hivi alifika mahali hapo pa ajali. Alisimama pamoja na wanawake wengine upande ule mwingine wa Barabara ya University uliokuwa umeinuka.Alipoona mkoba ule mdogo wa ngozi karibu na kitu kile kingine katikati ya barabara aliamini kwamba Boge pia alikuwa amehusika kwenye ajali hii. Mwanafunzi wa kike aliyempasha habari hii yamkini hakumwelezea kuhusu Boge.

> Mwanamke huyo alihangaika sana moyoni akitaka mtu amhakikishie ukweli wa jambo hilo. Hata hivyo, hakuthubutu kumwuliza yeyote kwa kuchelea kupata jibu la moja kwa moja kuwa:"Ndiyo Dora, ni kweli.Jamaa huyo pia alikufa (uk 60).

Kwa maneno haya, tayari msimulizi amezua hali ya taharuki kwa msomaji.Itakuwa bora kuendelea kusoma ili kutambua ni kwa nini Dora hashughuliki na jambo lingine lolote ila mawazo yake ni kwa Jay Boge. Hivyo, ikiwa msomaji ataendelea kusoma na kubainikiwa wazi na ukweli wa mambo kuhusu swali hilo, basi kwa mhusika huyo itaonekana kuwa kuna muala katika matini kupitia kwa mpangilio wa matukio yanayoonyesha wazi lengo la Dora. Katika ukurasa huo huo, Dora aliuliza;

> Hebu niambie, si yule pale ni Jay?"
>
> Msichana aliinamisha kichwa kama ishara ya kukubali na hata kabla ya kukiinua akaona Dora ametimua mbio kuvuka barabara, bila kujali magari yaliyokuwa sasa yameanza kwenda kasi kwenye barabara hiyo (uk 60).

Dora yuko radhi kuhatarisha maisha yake mwenyewe aking'ang'ania kumfikia Jay.

> Akiwa amevuka barabara salama na kupita katikati ya umati

ule, alikwenda mpaka mahali Boge aliposimama. Bila Boge kuona, Dora aliulizungusha mkono wake wa kushoto mabegani na kumvuta kutoka kwenye umati……. (uk 60)

Tukimfuatilia Dora zaidi, tunamkuta wakati anajizungumzia anapomchagulia Jay Boga shati, anasema;

Hili litaonekana maridadi akilivaa (uk 62).

Aliporudi garini na kumkuta Boge amelala aliamua kutomwamsha badala yake aliamua kurudi Barabara ya Queen Elizabeth ili amnunulie samaki pamoja na 'chips'. Hii ni ishara ya kujali maslahi ya mtu unayemthamini sana.

Tukiendelea kusoma, tunapata kuwa Jay Boge alipomwomba Dora kumpeleka nyumbani kwa akina Kanaya, Dora anakubali ingawa alikuwa amepanga kukutana na wanafunzi wake kwa mjadala alasiri hiyo. Baada ya mazishi ya Kanaya, Dora anaonyesha wazi kuwa nia yake ni kuchukua nafasi ya Kanaya katika moyo na katika maisha ya Boge. Dora anajitoa kumpeleka Boge kwake na anavyojipodoa katika matayarisho hayo ya kumpeleka, ni ishara kuwa ana nia maalum. Tunaambiwa, wanawake wengi hujipodoa lakini;

Tofauti iliyopo ni kwamba wale wenye nia maalum akilini huchukua muda mrefu zaidi kuliko wengine (uk 163).

Kwa jumla, matukio yanayomzunguka Dora yote yanamwelekeza kwa lengo lake la kumtaka Boge awe mpenzi wake. Huu ndio muala ambao umejitokeza na ambao unampa msomaji mwelekeo murwa hivi kwamba hata anaposoma ana uwezo wa kufasiri maana ya kila tukio.

### 2:4:3 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia mshikamano wa vipengele vya kiisimu katika matini pamoja na muala unaojitokeza kupitia taratibu mbalimbali. Katika kutalii taratibu za kiisimu, tumeshughulikia miundo ya nje ya matini na kuonyesha jinsi miundo hiyo inavyosukwa pamoja ili kuunda matini. Mshikamano wa kisintaksia unaojumuisha urejelezi, dhana ya udondoshaji wa vipengele, dhana ya njeo na kadhalika huchangia pakubwa usomekaji wa matini. Pale ambapo hapana upatanishi wa kiisimu unapata kuwa msomaji anakanganywa kila mara kiasi kuwa inambidi afikirie sana kila jambo ili kulioanisha na lingine. Matini ya namna hii huibua usomaji wa pole pole au hata kazi kutosomwa hadi mwisho. Kwa upande wa muala, tumeshughulikia uwiano wa maana zinazohusiana kuunda udhabiti wa matini

## SURA YA TATU

## 3.0 KAIDA ZA MATINI: WAHUSIKA WA KIMATINI

### Utangulizi

Usomekaji katika matini za kifasihi unaweza kushikamanishwa na uhusiano wa kimtazamo baina ya mwandishi na msomaji. Haijalishi ikiwa ni matini asilia au ni tafsiri. Usomaji wa kazi za tafsiri kama ulivyo usomaji wa kazi asilia, unabainika kutokana na kuzichunguza kaida za kimatini zinazoipa kazi tafsiri ukubalifu katika utamaduni unaohusiana na usomaji wa hadhira pokezi. Kimsingi, mtafsiri ni kiungo cha kimsingi kinachowezesha na kurahisisha mawasiliano katika hali ya uwingi lugha. Anauwezesha uelewano baina ya watu hasa katika hali zenye uwingi lugha na ungitamaduni. Jambo hili la kimawasiliano haliwezekani pasipokuwa na matumizi mwafaka ya vipengee vya kiisimu vya lugha pokezi. Lakini kabla ya matumizi ya vipengele hivyo, ni muhimu kwamba vipengele hivyo vitambulike tangu mwanzo. Hii ni kwa sababu vipengee vya kiisimu na vipengele vya matumizi ya matini, yaani vipengele vinavyowaingiza wahusika katika matini, ndivyo ambavyo humpa msomaji nafasi ya kuyafasiri mambo muhimu yaliyolengwa na mtafsiri.

Msomaji anaibua usomaji na ufasiri badalia kulingana na uyakinifu wa kazi husika na jinsi inavyotambua na kutumikiza vipengee vinavyokubalika katika ulimwengu wa mpokezi. Hii ndiyo sababu mtafsiri anahitajika kulielewa vyema suala zima la tafsiri ili aweze kufaulu katika uhawilishaji wa maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kaida anazohitaji kuzizingatia ni pamoja na lengo la mtafsiri, matarajio ya hadhira, hali zinazoizunguka matini tafsiri, yaliyomo, ukubalifu na hali ya mwingiliano matini.

Uhawilishaji wa maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine ni tukio muhimu mno linalomhitaji mtafsiri kuzingatia mambo muhimu. Sharti ahakikishe kuwa katika kazi yake mna ujumbe anaoupitisha kwa wasomaji. Ili asemekane kuwa amefaulu, msomaji anafaa kuisoma hiyo kazi na kuibua usomaji na ufasiri mpya ambao utamwezesha kuupata ule ujumbe ulionuiwa. Mambo haya yatategemea usomekaji wa matini. Ndiposa ni muhimu tukumbuke kuwa japo mazingatio ya taratibu za kiisimu ni muhimu wakati wa kutafsiri, mtafsiri hafai kujifunga kwazo tu mambo hayo ya kiisimu ikiwa kujifunga huku hakutawezesha kuwepo kwa mawasiliano. Hii ndio sababu Neubert, A na Shreve G. (1992) wanasema;

> Ni sharti mtafsiri aelewe vipengee vinavyoshirikiana kujenga matini ikiwa atavitumia kwa maslahi ya wasomaji wapokezi. Uchambuzi wa kiisimu wa matini inayotafsiriwa hauwezi kubaini kiwango chake cha umatini wa matini hiyo kikamilifu. Muundo wa kiisimu wa matini huibua mshikamano wa maarifa. Mshikamano huu wa maarifa ndio humchochea msomaji kukadiria umatini na kisha kuikubali matini. Yaani matini hujengwa kimsingi na vipengele vya lugha lakini matini hiyo huwa, haijafungika katika lugha hiyo kiasi cha kutoweza kuingizwa katika matumizi. Lugha ni kiwasilisho tu cha hali yake ya kuwa matini (uk 70).

Kutokana na mtazamo wa Neubert na Shreve, tunapata kuwa zipo kaida nyingine muhimu zinazojenga matini na kuwezesha usomekaji katika matini hiyo licha ya zile taratibu za kiisimu na muala. Katika sura hii, tutashughulikia kaida ambazo huchangiana na zile za kiisimu ili kuunda sifa changamano ya matini. Kaida hizo ni pamoja na; lengo la mtafsiri, ukubalifu wa matini husika, hali zinazoizunguka matini, yaliyomo na mwingiliano matini unaojitokeza. Hizi ni sifa ambazo zinaingiza mambo yaliyo nje ya

matini katika matini, na mambo hayo yanayoingizwa mbali na kuwa mambo ya kimsingi katika usomekaji, yanadhihirisha pia mahusiano ya wahusika wa kimatini; yaani mtafsiri, mpokezi /msomaji na tafsiri na ujumbe katika matini.

### 3:1 Lengo la mtafsiri

Kimsingi, mtafsiri yeyote huwa na lengo maalumu linalomsukuma kuhawilisha ujumbe fulani kutoka lugha moja hadi nyingine. Lengo hili lafaa kubainika katika matini kutokana na mshikamano wa mawazo unaoletwa na upatanishi wa vipengee vya kiisimu. Hivyo matini hujengwa na malengo ya mwandishi ambayo huathiri muundo wa matini yenyewe. Hivyo hivyo katika tafsiri, yaani wakati mtafsiri anapotafsiri hutaka kutimiza malengo fulani na hamu hiyo ndiyo ambayo humpa msukumo hadi akaunda matini yake. Kuna haja kutambua kuwa, lengo la mtafsiri wakati mwingine silo linalojitokeza katika mfumo mzima wa taratibu zilizounda matini husika. Hivi ni kusema kuwa aghalabu matini inaweza kuundwa na lengo fulani na usomaji wa matini hiyo hiyo ukaibua lengo tofauti kabisa. Neubert na Shreve (1992) wanasema hivi kuhusu swala hili;

> Wachunguzi wa matini huweza tu kubaini kile wanachokitambua kuwa kimo ndani ya matini hiyo. Isitoshe, dhamira ya msomaji anapochunguza matini ni kupata lengo linalojitokeza katika matini na sio lengo la mwandishi. Kulingana na mtazamo wa msomaji, lengo la matini linahusu ule uhusiano wa yaliyomo na hali yake; umuhimu wa ujumbe uliomo (uk 72).

Kulingana na maelezo hayo, tunaona kuwa lengo linaibuliwa na usomaji wa kazi iliyotafsiriwa. Basi wakati ambapo lengo limejitokeza, kazi husika husemekana kuwa inasomeka. Hali hii inajitokeza vyema katika *Madhabahu ya Kilio.* Watafsiri wa riwaya hii waliyaingilia maswala ya jamii

ya Kiafrika wakiwa na lengo la kuwazindua Waafrika kuhusu jinsi walivyokanganyikiwa kitamaduni. Wamelenga kuonyesha hadhira hali halisi inayoikumba jamii ya msomaji na ndiyo maana matini hii inasawiri mvuto kwa hadhira. Wamelenga kuyaingiza maswala haya ya kitamaduni katika jamii pokezi kutoka kwa lugha chanzi;

> Hadithi yake ni hadithi ya vijana wa Kilima wanaotafuta maana ya maisha yao katika tajriba zao za wakati uliopita na wa sasa. Ni hadithi inayohitaji kuhitimishwa ili nyingine ianze. Ni hadithi ya maswali yasiyojibiwa. Watamgeukia nani awaambie ukweli? Watamgeukia nani awape jibu? (uk 2).

Maneno haya yanaonyesha jinsi vijana hawa wamekanganyikiwa kuhusu mambo yanayowahusu na hawajui ukweli wataupata wapi kwa vile kila mtu katika Kilima hatambui jinsi mambo yanavyofanywa katika madhabahu ya kitaifa: Hili ni dhihirisho kuwa hapana mwelekeo au msimamo wa kitamaduni hata baada ya Waafrika kunyakua uhuru.

Katika mji mkuu wa Kilima kuna jumba lenye ukumbi wa sanaa za maonyesho ambamo vikundi vya waigizaji hukusanyika humo kuigiza michezo, muziki na ngoma. Maonyesho haya ya sanaa ndiyo kiunzi muhimu kabisa cha kukuzia utamaduni wa jamii yoyote ile lakini Waafrika wenyewe hawana uhuru wa kutumia ukumbi huo wapendavyo. Isitoshe, chuo cha Muziki cha Kilima kina wanachama wazungu pekee ambao ndio hukitumia kwa mazoezi ya muziki wa nyimbo za kirasimu. Je, ni utamaduni upi unaokuzwa katika nchi ya Kiafrika ya Kilima? Ili kutilia mkazo hoja hii hebu tazama maelezo;

> Madhabahu ya Kitaifa ya Kilima ni kitovu cha shughuli za kitamaduni cha wazungu na hivi karibuni hata Waeshia. Makundi ya kitamaduni ya

Kilima hukatishwa tamaa na kutumia chumba hiki kwa sababu ya ada za juu zinazotozwa. Hata hivyo wasanii na wasomi wenyeji hutumia baa iliyopo sehemu za juu kama makao yao makuu. Watangazaji, waigizaji wa kike na kiume, wanamuziki, waandishi wa magezeti, wahazili, wahadhiri na wanafunzi wa chuo kikuu huja hapa kukata kiu; kiu ya koo. Lakini wanapotaka kukata kiu nyinginezo, hasa kiu ya kitamaduni hawana budi kutafuta mahali pengine (uk 3).

Lengo la watafsiri hapa linajitokeza kuwa walinuia kuonyesha jinsi mwafrika asivyo na uwezo wala uhuru wa kudhibiti utamaduni wake. Juhudi zote zinazofanywa katika Kilima kuukuza utamaduni wa Wakilima zinadidimizwa. Ada zinazotozwa kwa kutumia madhabahu ya Kitaifa ya Kilima ni za juu sana kiasi kwamba makundi ya kitamaduni ya Kilima yanakatishwa tamaa. Wanaoweza kulipa ada hizi ni Wazungu hivyo basi utamaduni unaondelea kukuzwa ni ule wa Wazungu. Wanatumia chumba hiki kwa kuigiza michezo ya Kizungu na katika lugha ya Kiingereza. Orodha ya michezo iliyowekwa ukutani inadhihirisha jambo hili. Pia Wazungu waliwafanya Wakilima kuamini kuwa hawawezi kutenda mambo muhimu wenyewe. Hata walifanywa kuamini kuwa mwanamke mzungu ndiye mrembo. Katika tangazo la biashara la losheni iliyoitwa skino, Kanaya alikuwa ameshiriki lakini lilipotokea kwenye televisheni, Kanaya alishangaa;

> Katika tangazo hili, wanawake wengi weusi walikuwa wamegeuzwa nyuso zao kiujanja na kuwa kama za Wazungu
>
> (uk 63).

Haya yote yaonyesha ujanja wa mzungu katika kubadilisha nyoyo za Wakilima wajifikirie kuwa duni na hata waudharau utamaduni wao wenyewe.

Vikwazo na vizingiti vilivyodidimiza utamaduni wa Wakilima vinajitokeza kwa jinsi juhudi za Wakilima zinavyokatizwa. Kwa mfano, semina iliandaliwa huko Rinyet ili kuunda sera ya utamaduni katika Kilima lakini hati iliyoandikwa juu ya sera hiyo ilikufa tu isijulikane ilikwenda wapi. Huu ulikuwa ujanja wa Wazungu ili Wakilima wafikirie kuwa maendeleo yao yanatiliwa maanani. Kwa njia hii, wangejiendeleza tu bila Wakilima kujiuliza maswali. Hata hivyo, tunaona jinsi vijana wanavyoitilia shaka hali hii kupitia kwa mazungumzo yao.

Kupitia kwa mazungumzo ya vijana wasomi katika Kilima, Boge anawazindua vijana wenzake ili wajitafute na kung'ang'ania kuurudia utamaduni wao kwa kupigania kubuniwa kwa sera kamili ya utamduni wa Wakilima;

> Mwenzangu, ulichoona katika maktaba hiyo si sera ya utamaduni bali ni sheria ya zamani ya kikoloni ya utamaduni tuliorithi kutoka kwa wale wakoloni waliotutawala wakati tulipopata uhuru wa kisiasa (Uk 29).

Kuwahimiza vijana kutetea utamaduni wao anawaambia,

> Tunachohitaji kwa dharura ni sera kamili ya utamaduni na Wakilima wachanga wenye ujuzi na waliojitolea kuitekeleza kikamilifu sera hiyo hadi mwisho wake (uk 29).

Lengo la watafsiri hawa kwa hadhira yao limejitokeza barabara, yaani haja na ari ya kufikiria kwa makini jinsi wanavyoweza kuupa pumzi mpya utamaduni wao uliopotoka na kupotoshwa. Hali hii inazungumziwa vyema na

vijana wenyewe ishara kuwa haya ni mambo ambayo wanayaelewa. Hii ndiyo sababu usomekaji wa kazi hii unarahisishwa kwani maswala yanayojadiliwa yanajinasibisha vyema na hali halisi wanayoipitia wasomaji hivyo kuwapa mshawasha wa kutaka kusoma zaidi na kuelewa. Si mambo mageni kwao.

Haya ni baadhi ya mambo ambayo wasomaji wa Kiswahili wanatarajia kukumbana nayo katika matini hii. Matini hii ya *Madhabahu ya Kilio* imetafsiriwa katika kipindi cha baada ya ukoloni; wakati ambapo mataifa mengi yaliyotawaliwa yanaamka na kuanza kuzidadisi hali mbalimbali zinazowazunguka. Lugha za wenyeji zilizodharauliwa sasa zinajaribu kupata mwamko mpya huku utamaduni wa mzungu ukiendelea kusambaa na kuigwa kwa kiasi kikubwa, na utawala unafuata mikabala ya kikoloni na kadhalika. Hali hizi basi ndizo zinazoangaziwa na fasihi za mataifa kama haya, kwa hivyo watafsiri wanatarajiwa kuzipa matini za aina hii kipaumbele. Tafsiri za matini zenye ujumbe unaoyajadili mambo haya zinalenga kuwazindua Waafrika na kujaribu kupendekeza juhudi za kujikomboa kutokana na hali hii. Matini ya *Madhabahu ya Kilio* imebaini lengo hili hivyo kuonyesha uamilifu wake katika mfumo pokezi.

**3:2 Hali inayozunguka matini**

Lengo la mtafsiri ni mwongozo muhimu unaotoa matokeo mema ya kazi ya tafsiri, lakini lengo hilo peke yake halitoshi kuipa matini tafsiri ukubalifu unaofaa katika mfumo pokezi. Matini tafsiri huzalika katika mazingira ya kijamii, kihistoria, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimawasiliano, mambo ambayo huchangiana na lengo la mtafsiri kujenga ukubalifu. Hivyo, tukizungumzia hali inayoizunguka matini tuna maana ya kuiweka matini katika muktadha mahsusi wa kijamii, kitamaduni na kiwakati kwa misingi ya wakati maalumu na mahali maalum. Tukizingatia hoja hiyo,

jukumu la kimsingi kabisa la mtafsiri ni kuhakikisha kuwa matini ambayo inaibushwa na mtafsiri inampa msomaji nafasi ya kutambua hali ambamo matini inazalika. Yaani, mtafsiri sharti aelewe muktadha wa ujumbe anaoulenga kwa wasomaji wake, mitazamo yao, mahitaji yao na mazingira ya kijamii, kisiasa na hata ya kiuchumi.

Umuhimu wa kuiweka kazi tafsiri katika muktadha maalum unaotokana na utambuzi kuwa tafsiri ni njia muhimu katika ukuaji wa lugha na fasihi zote za ulimwengu. Mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni yameweza kuzikuza lugha zao na hata tamaduni zao kupitia kwa tafsiri. Wakoloni walipovamia bara la Afrika, walijifanya kuwasaidia Waafrika katika nyanja mbalimbali zikiwemo elimu, uchumi, siasa na kadhalika. Katika harakati hizo za ukoloni, wenyeji walifanywa kuelewa kuwa mzungu ni binadamu mwenye uwezo, lugha yake ni bora na kuwa lugha za wenyeji hazina thamani. Katika *Madhabahu ya Kilio,* Boge anaeleza jinsi walivyoadhibiwa vikali shuleni walipozungumza lugha zao za mama. Ilikuwa lazima wazungumze Kiingereza. Kwa hivyo *Madhabahu ya Kilio* ni kazi inayozalika katika mazingira ya taifa linaloibuka kutoka ukoloni, taifa ambalo licha ya kutokuwa na sera mahususi za kitamaduni, limo mbioni kujitoa katika tamaduni zinazolemaza akili za kikoloni.

Katika Bara la Afrika zipo tamaduni nyingi kama zilivyo lugha. Ili kuondoa kasumba kuwa zipo lugha bora na nyingine duni, ipo haja ya kutafsiri kazi mbalimbali kutoka lugha za Wakoloni hadi lugha za Kiafrika, kwa njia ambazo haziendelezi uelewa hasi wa hali za kikoloni. Baada ya ukoloni, Waafrika walitaka kujaribu kuinua hadhi za lugha zao na hapo pakazuka haja ya kuwa na matini zilizoandikwa katika lugha hizo. Basi tafsiri zilihitajika ili matini tafsiri zisomwe sambamba na matini asilia za lugha za Kiafrika. Shule nyingi katika Afrika ziliibuka na haja ya vitabu vya kusomwa

na katika Afrika Mashariki, tafsiri nyingi zilifanywa kwa lugha ya Kiswahili kwani ilizungumzwa kote. Hii ndiyo hali moja wapo ya zile zilizoibusha tafsiri katika lugha ya Kiswahili kutoka lugha za Kikoloni.

Maria Tymczko (1999) anatoa mfano wa msanii mashuhuri wa Kiafrika Ngugi wa Thiongo. Baada ya Ngugi kuandika riwaya nyingi katika Kiingereza, aligeuza mtindo na kuanza kuandika katika lugha yake ya mama Gikuyu. Alinuia kuendeleza lugha yake endapo kazi zake zingetafsiriwa katika Kiingereza na lugha nyingine za ulimwengu. Ni katika harakati na juhudi za kupigana dhidi ya lugha na tamaduni ngeni kutawala akili za Wafrika. Ngugi na wengine kama vile mshairi maarufu wa Ireland, Nuala Nidhomhncull wanapigania kutambuliwa kwa uwezo na nafasi za lugha zinazodaiwa kuwa ndogo ulimwenguni. Mfano huu unasisitiza umuhimu wa tafsiri kama mkakati unaoweka wazi hali za kibaguzi, unaoonyesha njia na uwezekano wa kuondoa fasihi katika hali duni; na zaidi kama mkakati wa kuzalisha uelewa na maarifa mapya. Kwa njia hii tafsiri za Kiswahili kutoka Kiingereza ni lazima zifanywe kwa njia ambazo haziendelezi maarifa hasi na ya kibaguzi. Tafsiri katika mkabala huu, ni mbinu na njia ya urekebishaji wa uelewa na ufahamu potovu wa mambo.

Hali nyingine inayohusishwa na kuibuka kwa tafsiri na ambayo inatambulika katika *Madhabahu ya Kilio* ni sababu zinazopelekea matini fulani kuchaguliwa na kutafsiriwa. Matini huweza kuchaguliwa kwa sababu kadhaa. Kwa mfano, matini zinazotoa fununu ambazo ama ni suluhisho kamili au zinaweza kuibua masuluhisho ya matatizo yanayozikumba jamii katika ulimwengu huweza kuzingatiwa. Pia, matini yaweza kuchaguliwa kwa sababu inawakilisha eneo fulani la utamaduni au fasihi hivyo kuweza kuendeleza utamaduni na kushinikiza ugunduzi wa vipengee vya kiutamaduni ambavyo huchangia ukuaji wa lugha, fasihi na utamaduni mahususi wa watu.

Kilima ni nchi inayowakilisha mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni. Kwa sababu ya sera hasi za kikoloni, ujanja wa mishenari pamoja na ugandamishaji wa utamaduni na asasi za Kiafrika, Wakilima wakafunzwa pia kudharau kila kilichokuwa chao. Wenyeji wa Afrika waliiga utamaduni wa mkoloni na kusahau utamaduni wao kwa kuwa walifunzwa kutojiamini. Walifunzwa elimu ya mkoloni kupitia kwa lugha ya mkoloni na ndani ya elimu hiyo wakafunzwa falsafa za kutojiamini au kuamini uwezo wao. Baada ya mataifa haya ya Kiafrika kupata uhuru, ilikuwa ni kama walipata uhuru wa bendera tu kwa sababu utamaduni wa mkoloni bado ulitukuzwa wa Kiafrika ukasahaulika. Ingawa walijaribu kuunda sera zao wenyewe za kuziendeshea shughuli zao, walikuwa wamejazwa kasumba ya kudharau juhudi zao wenyewe na kutukuza za wakoloni. Tunaambiwa kuwa mzungu aliyeingia katika baa ya Hell's Gate aligeuza hali humo.

> Wahudumu wote wa kike kwa pamoja walipiga makofi huku wakikimbilia na kumkumbatia na hata kumbusu yule mzungu... (uk 84).

Hali hii inayobainika katika mataifa mengi ya Kiafrika baada ya uhuru ndiyo inayoizunguka matini ya *Madhabahu ya Kilio.*

Juhudi za kubuni sera ya utamaduni ili kuukuza utamaduni wa Kilima zilididimizwa pale ambapo fedha zilitumiwa kuandaa semina ya Rinyet kushughulikia swala hilo na baadaye hati iliyoandikwa ikadidimia. Katika madhabahu ya Kitaifa, katika filamu iliyoigizwa na wazungu, Hedimasta alikuwa amepewa nafasi kubwa ya mhusika mweusi iliyochukua muda wa dakika saba au nane katika jumla ya saa mbili za filamu hii. Uwezo wote wa kijamii, kitamaduni na kadhalika ulishikiliwa na wazungu katika nchi ya

Kilima. Ni wazi kuwa wazungu waliwajaza Wakilima kasumba ya kutojiamini.

Mjadala huu unatupa mwelekeo fulani kama wasomaji, kwamba matini ya *Madhabahu ya Kilio* imechangia upanuaji wa maarifa na tajiriba za kimaisha kwa hadhira pokezi. Vile vile imejaribu kuleta uzindushi kwa hadhira pokezi pamoja na kukuza lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa taratibu za kiisimu zilizotumiwa ili kuweza kubainisha wazi hali inayoizunguka matini ya *Madhabahu ya Kilio*.

### 3:3 Yaliyomo

Ili msomaji na mtafsiri waweze kuwasiliana lazima pawe na habari ambazo zinajulishwa kwa msomaji. Ikiwa matini haisawiri habari muhimu ambazo msomaji anahitaji kuzijua basi matini hiyo huwa imepungukiwa kwa upande wa maudhui. Hali ya kumjuvya msomaji kuhusu habari fulani ni kigezo muhimu au cha kimsingi cha kupimia umuhimu wa tafsiri. Mtafsiri ana jukumu la kumjuvya msomaji wake kuhusu matukio na mambo muhimu yanayopatikana katika matini asilia.

Mambo muhimu yanayozungumziwa katika matini hutegemea hali inayoizunguka matini husika. Hivyo matini ambazo huzalika katika hali moja zinaweza vile vile kusawiri maudhui au habari za namna moja. Hata hivyo maudhui hujitokeza tu katika matini kulingana na jinsi yanavyombainikia msomaji. Hivyo mtafsiri anapounda matini yake lazima atumie lugha kwa njia inayoweza kumpa msomaji nafasi ya kutambua yaliyomo. Kwa njia hii, matini itaonyesha usomekaji wa hali ya juu kwani si jambo la kawaida kwa msomaji kuendelea kusoma maandisi yoyote yale ikiwa haelewi au hafahamu mambo yanayojadiliwa na umuhimu wake kwake.

Katika *Madhabahu ya Kilio*, maudhui yamejitokeza kwa njia ya wazi kabisa hivyo kumhamasisha msomaji kuendelea kusoma. Hali hii inaambatana na hoja kuwa yaliyomo yanaoana na mambo ambayo msomaji anayapitia katika maisha. Maudhui ya utamaduni wa Mwafrika pamoja na jinsi Mwafrika huyo ameiga mengi yahusianayo na utamaduni wa mkoloni yamejadiliwa kwa kina. Tunaona juhudi za Mwafrika kutaka kuukuza utamaduni wake kwa kujenga majumba yenye ukumbi wa sanaa za maonyesho. Jengo hili la Kilima lilinuiwa kusaidia vikundi vya kitamaduni vya wananchi wa Kilima kuigiza michezo yao, miziki na ngoma. Kwa njia hii utamaduni wao ungeendelezwa. Lakini jambo la kusikitisha ni kuwa jumba hili aghalabu linatumiwa na Chuo cha muziki cha Kilima, chenye wanachama wazungu pekee, kwa mazoezi ya muziki wa nyimbo za kirasimu. Utamaduni wa Mwafrika unadidimizwa katika Afrika na Waafrika wenyewe ndio wanaoutukuza utamaduni wa mzungu.

Hali hii ina misingi yake katika historia ya Kilima kama nchi iliyotawaliwa na Wazungu. Wakati wa mkoloni, Mwafrika alipokonywa mamlaka yake, mali na ardhi. Vyote vikawa vya Mzungu. Wazungu walimiliki uwezo wa kisiasa, serikali na sheria, utamaduni na lugha. Athari ya haya yote ilikuwa, Waafrika Wakilima kuurithi utamaduni, lugha, siasa na kadhalika kutoka kwa Mzungu. Hivyo baada ya ukoloni mambo haya yaliendelezwa na viongozi waliochukua hatamu za uongozi. Kwa njia hii uzungu ulipata nafasi ya kuendelea hivi kwamba asasi nyingi bado zilimilikiwa na kutawaliwa na Wazungu, ambao wana uwezo wa kiuchumi, wa kisiasa, wa kielimu na hata wa kitamaduni dhidi ya Wakilima. Hata lugha na fasihi ya Wazungu ndiyo inayokuzwa. Boge anasema kuwa wakiwa shuleni walilazimishwa kuzungumza Kiingereza pekee na katika jumba la kuigizia michezo, Wazungu ndio wanaochezea hapo michezo ya Kizungu.

Vifaa ambavyo vinatumiwa katika sherehe ni vile vya mkoloni. Kwa mfano, katika sherehe ya kumkaribisha yule kijana wa Kiingereza, kulikuwa na vibilauri vidogo vidogo ambavyo vishikio vyao vilikuwa kama nyigu. Hizi ni bilauri zilizoletwa na ukoloni wala sio vifaa vya Kiafrika. Isitoshe, vyombo vya habari vilitilia maanani utamaduni wa mkoloni.Tunaambiwa;

> Soita alikuwa amealikwa rasmi kwenye karamu kama mtayarishi mashuhuri na mkurungenzi wa kipindi cha mambo ya kitamaduni kilichokuwa kikionyeshwa kila wiki kwenye televisheni ya kitaifa. Kipindi chenyewe kilionyesha mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali kutoka nchi zinazojulikana kama nchi zilizoendelea na zilizokuwa na uhusiano wa kibalozi na Kilima (uk 5).

Vile vile, yale mabango yaliyokuwa yametundikwa ukutani katika Madhabahu ya Kitaifa ya Kilima yalikuwa yameorodheshwa michezo ya kigeni. Huu ni utamaduni wa mkoloni uliokuwa ukikuzwa huku wa Mwafrika ukididimizwa. Hii ni kwa sababu ya uwezo hasa wa kuitamaduni waliokuwa nao Wazungu dhidi ya Wakilima ambao walifanywa kuamini kuwa lugha yao pamoja na utamaduni wao ni duni.

Jambo jingine muhimu ambalo limeshughulikiwa humu ni kuendelezwa, kudumishwa na kuhifadhiwa kwa utamaduni wa Kiafrika. Katika matanga ya Kanaya, ilikuwa muhimu kuwa pawe na moto wa maombolezo kama unavyodai utamaduni wa jamii hiyo. Wakati maiti ya Kanaya ilipokuwa inasafirishwa kwenda nyumbani kwa mazishi, umuhimu wa utamaduni ulidhihirika. Sura ya 16 inadhihirisha nyoyo za jamaa kuwa maiti ya Kanaya imerudishwa mahali ambapo kiunga-mwana chake kilizikwa alipozaliwa. Wanaamini kuwa gari ambalo limebeba maiti ndilo huachwa liongoze njia wakaribiapo nyumbani eti kuwa roho yake inajitafutia njia. Hizi

ni mila na desturi za jamii ya Kanaya ambazo wazee waliziona kuwa ni muhimu. Mioto mitatu ya maombolezo pia iliwaka hadi baada ya mazishi ya Kanaya kama ilivyokubalika kulingana na mila. Haya ndiyo mambo yaliyoridhisha watu wa jamii hiyo.

Taratibu hizi si taratibu za kishenzi bali ni imani ambazo zimeikuza na kuilea jamii hii. Kwa hivyo, swala la utamaduni linalozungumziwa hapa linalenga kuonyesha jinsi utamaduni mmoja unavyokandamiza mwingine. Kwamba mahusiano ya Wakoloni na waliotawaliwa hayakujitokeza tu katika daraja ya utawala na siasa, bali pia katika utamaduni. Kwa usemi mwingine, madhara makubwa zaidi ya ukoloni ni yale ya kitamaduni, kwa sababu yanaendelea kudumu miaka mingi baada ya kupatikana uhuru wa bendera. Haya ndiyo mambo yanayoiwezesha kazi hii kukubalika na kusomeka katika lugha na fasihi pokezi kwa jinsi yanavyojinasibisha na hali halisi ya wapokezi.

Swala la kutowajibika kazini miongoni mwa washikilia nyadhifa za uongozi na utawala limeshughulikiwa kama linavyodhihirika hata sasa katika mataifa yanayoendelea ya Kiafrika. Barabara zimeharibika na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kurekebisha hali hiyo na watu ambao wamepewa jukumu hilo katika serikali. Mheshimiwa Mbagaya ambaye ni mbunge wa sehemu ya akina Kanaya anasemekana kuwa huongea wakati wote juu ya maendeleo na ustawi kwenye redio bali ameshindwa kutengeneza barabara za eneo lake. Pia makubaliano yaliyofanywa hapo awali ya kubuni sera ya kulinda utamaduni wa watu wa Kilima, pamoja na kwamba yaliandikwa katika hati fulani, yalididimia tu yasionekane au kuzingatiwa. Kutowajibika huku ni tatizo ambalo linafaa sana kuangazwa na fasihi ya jamii yoyote ile hivyo, ni swala muhimu ambalo matini tafsiri ya *Madhabahu ya Kilio* imeliingiza katika mfumo pokezi.

Umaskini wa Wakilima ulichangia pakubwa kutoendelea kwao katika nyanja mbalimbali za maisha. Umaskini huu una misingi yake katika historia. Wazungu walipoyaingilia maswala nyeti ya bara la Afrika Kilima ikiwemo, walitumia rasilimali ya Waafrika kujitajirisha huku wakimwacha Mwafrika akiwa hana lolote ila kumtegemea Mzungu. Ardhi ndiyo rasilimali muhimu ya kuendesha shughuli za ukulima ambazo ndizo uti wa mgongo wa uchumi wa mataifa mengi ya bara la Afrika. Hivyo ardhi ya Waafrika iliponyakuliwa, ni wazi kuwa uwezo wa kuzalisha mali uliwaendea Wazungu. Kuanzia nyakati hizo, Waafrika walifanywa kuamini kuwa wao hawana uwezo wowote na kwamba hawawezi kuendelea bila Mzungu. Hali hii iliwarudisha nyuma sana kimaendeleo. Umaskini huu ndio uliowafanya wasiuendeleze utamaduni wao katika jumba la kuigizia michezo kwa vile walishindwa kulipa ada za juu zilizotozwa kutumia jumba hilo. Walijisikitikia na kujiona duni; hali ambayo iliwafanywa wasijiamini. Kwa sababu hii Waafrika wanakumbwa na matatizo mengi ya kiuchumi kiasi kwamba uwezo unabaki tu kwa Wazungu ambao wanatenda wanavyotaka kama katika nchi ya Kilima.Hali hii imezikumba nchi nyingi hasa katika kipindi cha baada ya ukoloni na ndiyo maana matini tafsiri ya Madhabahu ya Kilio ina nafasi yake katika mfumo mzima wa wapokezi.

Maendeleo ya nchi hutegemea uwezo alionao mwananchi kama anavyodai Batten, T.R. (1960) anaposema;

> Hakuna watu wanaoweza kufikia au kuthibiti uhuru unaofaa hadi wanapoweza kuzalisha mali mathubuti kuwakidhia mahitaji yao ya kimsingi (uk76 ). (Tafsiri yetu)

Batten naye aliufungamanisha mtazamo wake na dhana kuwa binadamu asiyeridhika kwa kunyimwa maisha mazuri ya kijamii, elimu mwafaka,

nidhamu ya kibinafsi ya kuweza kufanya kazi na jamii thabiti kutokana na hali ya kiuchumi, hawezi kutarajiwa kuthibiti maisha yake mwenyewe au ya taifa lake. Badala yake atakuwa chini ya ukatili wa kisiasa na kiuchumi.

Hali hii ndiyo inayowaweka Wakilima katika hali wanamojikuta ya kuendelea kudumisha sera, kaida na mifumo hasi ya kikoloni. Hata hivyo, hali hii inatiliwa shaka na Wakilima wanaong'ang'ania kujidadisi na kutafuta mwelekeo unaoweza kuwarudishia heshima yao. Hivyo tafsiri za matini zinazoyajadili maswala haya katika awamu hii ya baada ya ukoloni zina mchango kwa hadhira pokezi kwa jinsi zinavyoridhisha mahitaji na matarajio yao. Hadhira pokezi inaibua usomaji na ufasiri mpya katika lugha pokezi hata isipokumbana na matini asilia. Kwa njia hii usomekaji unahimiliwa na misingi ya kuaminika na kukubalika miongoni mwa wasomaji wa matini tafsiri. Ni kazi ambayo inaleta matumaini kwa wasomaji kwa sababu ya uzindushi unaojitokeza miongoni mwa vijana ambao wameanza kujiuliza maswali kuhusu hali yao na kama Boge asemavyo, wanachohitaji kufanya ni kujitolea kupigania sera zao wenyewe kwa bidii. Wasomaji wanahitaji ari ya namna hii kwani wanaogelea katika mkondo wa maisha ulio sawa na huu wa Wakilima.

Watafsiri walikuwa wamekumbana na mambo haya muhimu katika matini chanzi kisha wakafahamu vyema kuwa ni mambo yanayoweza kuwafaidi wasomaji katika lugha pokezi. Kwa sababu, hii mchango wanaouleta katika maisha ya wapokezi haufai kupuuzwa. Kutowajibika kazini ni jambo ambalo limeirudisha nchi ya Kilima nyuma kimaendeleo. Uchumi hauwezi kuinuka pasipo uwezo wa kisiasa, kielimu na kitamaduni. Kwa hivyo watafsiri hawa wamejitokeza kama kiungo muhimu kati ya wasomaji na hali halisi ya ulimwengu wa wasomaji hao. Lazima Wakilima wajifikirie, wabadili

mienendo yao ili waweze kuinua uchumi wa nchi yao. Ufasiri wa mambo haya ya kihalisia unaipa kazi hii uthabiti ambao ni kipengee muhimu sana katika dhana ya usomekaji.

Vipawa miongoni mwa vijana katika nchi ya Kilima havikuzwi jinsi inavyostahili. Vijana wakisaidiwa na serikali, wanaweza kujisaidia katika ulimwengu huu uliojaa ukosefu wa kazi. Tunapata kwamba wale ambao wana vipawa wanakatizwa tamaa wakati ambapo wazungu wanapewa kipaumbele kuendeleza uwezo wao katika nyanja mbalimbali. Boge na Kanaya ni Wakilima ambao walikuwa na vipawa chungu nzima. Boge alikuwa mwigizaji bora zaidi katika shule za nchini na hata aliweza kushinda tuzo kadhaa. Wapo vijana wengine kama vile Jopa Juma, Mubina Kabina na wengine ambao walikuwa wasanii walioshiriki katika michezo katika Chuo Kikuu cha Kitaifa. Vijana hawa wote hawakuhimizwa kuendeleza vipawa vyao badala yake wazungu ndio walifaidika. Kwa wakati mmoja vijana hawa walionyesha kuchanganyikiwa na mtazamo huu wa serikali yao na kuonyesha mwamko wa kimawazo unaofaa kuigwa na vijana katika bara la Afrika.

Tunaelezwa kuwa, wakiwa wameketi walipitikiwa na mambo mengi akilini mwao;

> Ulikuwa mtindo tangu miaka ya hamsini kwamba mojawapo ya vikundi vya wazungu waigizaji kilipotoka kuonyesha igizo kubwa kwenye madhabahu, wangetafuta mwendeshaji michezo au mwigizaji mashuhuri, ambaye ni Mwingereza ili aje aongoze uigizaji au achukue nafasi ya muigizaji mkuu...... (uk 12)

Katika ukurasa huo huo tunaelezwa pia kuwa vijana hawa hawakufurahishwa na jambo hilo la wazungu kusaidiwa kuendeleza utamaduni wao katika nchi ya Kiafrika. Msimulizi anasema hivi;

> Ingawa walikuwa wachovu na wenye kiu, yale maandishi "meupe" kwenye ukuta mweusi nyuma ya kaunta yaliwakera. Waliketi pale kwa muda mrefu wakijadili maana hasa ya majina ya wazungu kwenye ukuta ule mweusi katika Madhabahu ya kitaifa ya Kilima, nchi iliyo huru kisiasa na kitamaduni (uk 12).

Matokeo ya haya yote yalikuwa ni kukata tamaa kwa vijana hawa na hivyo kutoweza kukuza vipawa vyao. Mambo haya yana umuhimu kwa hadhira pokezi kwani yanaiwezesha kuyatumia kuzidadisi hali zao na kujaribu kutafuta suluhisho. Na huu ni mchango mkubwa ambao umewezeshwa na matini tafsiri ya *Madhabahu ya Kilio* hasa katika kipindi hiki ambapo vijana wamekosa mwelekeo.

Swala lingine nyeti ambalo limejadiliwa katika riwaya hii ni ubadhirifu wa viongozi wanaosimamia idara mbalimbali katika Kilima. Tunapoelezwa kuhusu shughuli ya Rinyet ya kuunda sera iliyofaa ya utamaduni kwa nchi ya Kilima, tunachohisi ni uharibifu mkubwa wa mali ya umma. Tazama fedha zilizotumiwa katika shughuli hiyo ambapo wazalendo walijitolea kwa wingi kujaribu kuunda sera ya ustawi wa utamaduni wa nchi yao changa. Zilitumiwa fedha nyingi mno kutoka kwa serikali kugharamia shughuli hiyo lakini mradi wenyewe haukufaulu. Baada ya majadiliano, hati yenyewe ilikutana na kifo chake kisichotarajiwa kama alivyosema Kanaya. Haya ni baadhi ya mambo ambayo mtafsiri aliyaona, kuwa ya maana sana na ya uzindushi kwa wapokezi wa matini hii *Madhabahu ya Kilio*.Tunaelezwa;

> Hiyo ni sifa ya Kilima. Aliyeiua hati hiyo huenda tusimjue (uk 33).

Wakilima wanashirikishwa katika shughuli hii ambayo iliharibu fedha nyingi mno za serikali na haikufaulu. Huu ni ujanja wa kuwafanya Wakilima kufikiria kuwa shida zao zinatiliwa maanani.

Mifano mingine ya ubadhirifu inajitokeza wakati wa mahojiano ya Boge na Mheshimiwa Gasia. Watu wengi waliletwa kutumia mali ya umma eti kwa sherehe za kitamaduni.

> Habari iliyoandikwa kwenye gazeti la pili ilitilia mkazo jinsi sherehe hizi zilivyokuwa zimeandaliwa vizuri. Mfano ulitolewa kuonyesha jinsi waandishi wa habari walivyoshughulikiwa vyema. Hasa namna ambavyo mwandishi wa habari hiyo alivyopatiwa usafiri bila kutarajia, kwenda na kurudi hotelini.(uk 42).

Sherehe hizi za tohara zinadhaminiwa kwa fedha nyingi mno ilhali Kilima ni nchi ambayo uchumi wake, haujapiga hatua inayoweza kuridhisha. Wanadanganywa kuyatilia maanani mambo yasiyo na maana.

Suala la wingine limejitokeza katika *Madhabahu ya Kilio* kwa jinsi suala la wanawake linavyojadiliwa ingawa utamaduni wa Wakilima unatetewa dhidi ya utamaduni wa Wazungu. Ni wazi kuwa nafasi ya mwanamke bado inatiliwa ubaguzi wa aina moja au nyingine. Kwa mfano, ni kundi la watu waliopo bila kutambulika katika nyanja muhimu za kimaisha. Wanaume ndio ambao wamepewa uwezo wa kusimamia asasi mbalimbali za serikali. Katika siasa, tunapata waheshimiwa wa kiume tu pekee kama vile Mbagaya na Gasia. Katika mambo ya kitamaduni, tunapata kuwa hedimasta ambaye ndiye anayepewa nafasi katika uigizaji wenye wanachama wa kizungu tu ni mwanamume. Wanawake wengi katika kijiji cha Seboa hawana nafasi muhimu au za juu katika siasa.

Hata hivyo, wapo wahusika wa kike ambao wamepewa nafasi katika elimu, kama vile Kanaya, Kamonya, Vanity na wengine. Lakini kwa jumla hawajapewa uwezo wa kushiriki katika masuala muhimu. Vile vile hii ni jamii ambamo wanaume ndio wengi wakilinganishwa na wanawake. Hii ni mojawapo ya mambo ambayo yaliwasukuma watafsiri kutaka kuwazindua wasomaji wa Kiswahili ili kuyatafakari na kujaribu kuchukua hatua kwayo.

**3:4 Ukubalifu**

Dhana ya ukubalifu katika matini katika mazingira mahsusi inafungamanishwa na lengo la mwandishi. Lengo la mwandishi haliwezi kutimizwa ikiwa kazi inayohusika haimpi msomaji nafasi ya kulitambua lengo hilo. Ukubalifu hauna maana tu ya msomaji kuwa na mtazamo sawa wa kiitikadi na yaliyomo bali inamaanisha kuwa msomaji anaweza kubaini au kutambua yaliyomo. Huu ni mtazamo unaozingatiwa na wataalam Neubert, A. na Shrere. G. (1992) wanasema;

> Ukubalifu haumaanishi tu kuwa mpokezi anayaamini yaliyo katika matini. Unamhitaji mpokezi aweze kutambua yaliyomo. (Uk 73). (Tafsiri yetu)

Hakuna sheria au kanuni ambazo zinahusiana na ukubalifu bali aina mbalimbali za matini zina vigezo mbalimbali ambavyo huipa matini hiyo ukubalifu wake. Ikumbukwe kuwa matini zote aghalabu huonyesha kiwango fulani cha ukubalifu. Hivyo jukumu kubwa la watafsiri limekuwa; kuhakikisha kuwa matini wanazozitafsiri zinakubalika na hadhira pokezi ambayo haielewi kaida zinazojenga matini asilia.

Mtaalam Grice (1975 ) alizua dhana ya ushirikiano katika mawasiliano ya aina yoyote yale. Yaani palipo na mawasiliano ya aina yoyote, lazima wahusika washirikiane kwa kiasi kikubwa. Katika mawasiliano ya moja kwa moja, inambidi msomaji au mwandishi kuhakikisha kuwa anaeleweka. Vivyo hivyo, mtafsiri ambaye ndiye kiungo kati ya wazungumzi wa lugha chanzi na lugha pokezi lazima ategemee ushirikiano huu ili awasiliane na hadhira pokezi. Basi usomekaji wa kazi hiyo iliyotafsiriwa utategemea kiwango cha ushirikiano huo (kiwango cha uelewekaji wa kazi yake).

Neubert na Shreve wanasema;

> Matini ni mwaliko wa kushiriki katika mawasiliano na hii ina maana kwamba ni lazima matini zibuniwe, zijengwe na kuwashilishwa kwa wasomaji kwa njia zinazowawezesha wasomaji kushiriki katika kuzisoma na kuzifahamu. (uk 45)

Ni sharti matini ibuniwe katika misingi inayodhihirisha vipengee vinavyohimili matini yenyewe na vinavyomvutia msomaji kujiingiza na hata kubakia katika mawasiliano katika matini hiyo. Kaida ya ushirikiano inaeleza uwezo wa msomaji wa matini iliyotafsiriwa kutambua maana ya matini na hata kuikubali. Utambuzi huu unawezekana hata pale ambapo mwandishi wa matini asilia hajulikani wala hakunuia matini yake kwa hadhira ya kazi iliyotafsiriwa. Dhana ya ushirikiano huchangia usomekaji kwa njia nyingi hasa kwa kuwa uelewekaji wa kinachosomwa ni lazima uchangiwe na kiasi cha yaliyomo, ubora wa maandishi, uhusiano unaojengwa kati ya mtafsiri na msomaji pamoja na aina ya diskosi au mwelekeo wa matumizi lugha unaojitokeza katika kazi tafsiri. Mambo haya ya ushirikiano yanajitokeza katika *Madhabahu ya Kilio* kwa njia nyingi na hii ndio sababu kazi yenyewe inaeleweka.

### 3:4:1 Kiasi cha yaliyomo

Aghalabu, waandishi wa matini asilia wanapojenga matini zao huwalenga wasomaji katika lugha na utamaduni asilia. Vivyo hivyo mtafsiri anapotafsiri kazi yoyote huwa anawalenga wasomaji katika lugha pokezi ambao anatambua kwamba ufahamu wao wa matini anayoitafsiri utachangiwa na uhalisi wa lugha, fasihi na utamaduni wanamopatikana. Ufahamu huu ndio unaomfanya mtafsiri kutambua wajibu wake kwa msomaji anapobadilisha mpangilio wa maneno, kupunguza au hata kuongeza maelezo ili kufidia mahitaji ya wapokezi. Hii ni kwa sababu ya tofauti za kiisimu, miundo ya lugha, mfumo wa kazi nzima pamoja na matarajio ya hadhira pokezi. Maana inayokusudiwa katika matini asilia yaweza kukosa maana katika mazingira ya matini pokezi. Kwa hivyo, kaida hii ya kipimo humpa mtafsiri mwelekeo anaohitaji ili kuhakikisha kuwa taarifa anazozitoa ndizo zinazohitajika katika mazingira ya wapokezi.

Jinsi mtafsiri anavyopanga taratibu za kumwezesha kuyafikia mawasiliano, huwa anampa msomaji nafasi ya mbele zaidi. Hii ni kwa sababu inawezekana hadhira pokezi itarajie kukumbana na taratibu fulani za lugha au za kisarufi. Kule kupunguza maelezo au kuyabana katika mfumo mwafaka wa mawasiliano ndiko kunakoleta muala katika matini na kuteka makini ya msomaji kiasi cha kumfanya aikubali kazi yenyewe. Hii ni kwa sababu, zipo taratibu fulani katika lugha chanzi ambazo zaweza kukosa maana katika lugha pokezi. Na hivyo inawezekana kuwa maelezo yanayodondolewa hayahitajiki na msomaji.

Vile vile kaida hii huhusika katika suala zima la uteuzi wa maneno kileksika katika tafsiri. Yaani wakati mwingine matini asilia huwa na maneno ambayo yana maana tu katika utamaduni wa hadhira chanzi. Katika hali hii, mtafsiri anaweza kuamua kutumia ufafanuzi badala ya kuhamisha neno vile lilivyo kwani huenda lisilete maana yoyote kwa hadhira pokezi. Mchango wa mtindo huu ni kuwa unawezesha kupatikana matini zilizotafsiriwa ambazo ni pana au finyu zaidi kuliko matini asilia; jambo ambalo haliwezi kuepukika hasa pale hadhira pokezi inapotiliwa maanani. Katika *Madhabahu ya Kilio*, ipo mifano mingi inayohusishwa na kaida hii hivyo kupelekea matini kuthibitisha kiwango fulani cha usomekaji.

Ipo mifano ya ufafanuzi uliotolewa kuhusu dhana fulani katika Kiingereza ambazo hazingeleta maana yoyote kwa msomaji iwapo zingehamishwa jinsi zilivyo.

Kiingereza: "Nurses' swimming pool"
Kiswahili: "Kidimbwi cha kuogelea cha wauguzi"

Kiingereza: "Emptiness number thirteen"
Kiswahili: "Ukosefu wa maana katika maisha nambari Kumi na Tatu".

Kiingereza: "Spine"
Kiswahili: "Uti wa mgongo"

Kiingereza: "For the next two hours, Boge walked…."
Kiswahili: "Kwa muda wa masaa mawili yaliyofuata alitembea"

Kiingereza: "Fire of tears"

Kiswahili: "Moto ule maalumu wa maombolezi" (uk 76).

Ingawa katika Kiswahili tunakumbana na maelezo marefu, inaeleweka kuwa miundo ya kisarufi na kileksika ya lugha ya Kiswhaili imezingatiwa. Mtafsiri anaposema "Ukosefu wa maana katika maisha Nambari Kumi na Tatu" kwa maana ya "Emptiness Number Thirteen" ametumia mtindo wa ufafanuzi ili msomaji aweze kuelewa maana ya ujumbe. Ikiwa mtafsiri atajali tu kutosheleza muundo wa lugha ya Kiingereza aseme "Utupu nambari Kumi na Tatu," msomaji hatang'amua maana hasa ya kauli hiyo. Vile vile, "Moto ule maalum wa maombolezi" ni maelezo marefu mno kwa "Fires of tears". Lakini je, kwa msomaji wa Kiswahili, kutafsiri "fires of tears" kama "moto wa maombolezi" ni jambo lisiloonyesha dhana ya umahususi wa moto kwa msomaji. Hata hivyo kauli hizo mbili zinajitokeza kama lugha ya kiishara ambayo inafaa kutafsiriwa kwa kutafutiwa visawe katika lugha pokezi. Hivyo, ingawa mtafsiri ametumia maelezo marefu, hayo ndiyo mambo yanayohitajika ili msomaji aelewe ujumbe ulionuiwa na hivyo kutuwezesha kukata kauli kuwa hii ni kazi ambayo inasomeka kwa mujibu wa mahitaji ya hadhira pokezi.

Newmark Peter (1988) anasema kuwa endapo lugha ya kijazanda imetumiwa, aghalabu huwa inaleta picha ya ulinganisho wa vitu vinavyofanana au kukaribiana sana kwa sifa fulani. Na kuhusu tafsiri ya lugha ya aina hii anasema;

> Hapa, kwa upana, mtafsiri ana uhuru wa kuchagua tafsiri ya moja kwa moja akimwachia msomaji nafasi ya kuyatafakari. (uk 10)

Kwa hivyo, watafsiri wa *Madhabahu ya Kilio* walivyotafsiri kauli hizi mbili, msomaji ana hiari ya kusoma na kuibua ufasiri badalia kwa kuchukulia kuwa "Ukosefu wa maana katika maisha nambari kumi na tatu" kwa upande mmoja unaleta picha ya maisha kukosa maana na " Moto maalum wa maombolezo" kwa upande mwingine inaleta picha ya moto ambao unawashwa tu palipo na matanga. Hivyo basi, haya yanayojadiliwa hayatupi lolote la ziada bali dhana muhimu tunazotarajia, tuwe tumekumbana na matini asilia au la. Kimsingi, hizi ndizo baadhi ya taratibu au kaida za kimatini zinazoiwezesha kazi kusomeka hasa zinazompa msomaji nafasi ya kuibua usomaji na ufasiri unaoafikiana na matarajio yake katika lugha na fasihi pokezi. Na ikiwa kiasi cha yaliyomo kinalenga kuwezesha uelewa wa dhana muhimu katika matini basi usomekaji wa matini hiyo huafikiwa katika hadhira pokezi.

**3:4:2 Kaida ya ubora**

Kaida ya ubora inadai kuwa katika mawasiliano, mzungumzaji au mwandishi sharti azingatie uhalisi wa yaliyomo ili ukubalifu wa mambo yanayogusiwa utimizwe. Uhalisi huu utajitokeza kulingana na ithibati zilizoko zinazouhimili ukweli huo. Ukweli unaojinasibisha na hali halisi ya maisha katika ulimwengu tunamoishi. Lyons (1977) anasema;

> Kusema kuwa kauli zinazoeleza hali ya mambo ni mojawapo ya uamilifu wa lugha. Kuwa, kunatumiwa kama ilivyo kanuni zetu nyingine na ruwaza za kihulka katika kuunda na kudumisha mahusiano ya kijamii na kwa maelezo ya mitazamo yetu na ubinafsi wetu. (uk 50)

Hivi ni kusema kwamba matini hubeba maana zilizo katika muala maalumu unaoeleza mambo yanayohusu vitu, hali, matukio au shughuli zinazohusiana na ulimwengu halisi. Muala huu huchangiwa na matumizi bora ya vipengee vya kiisimu kama tulivyojadili vikiwemo viunganishi, viwakilishi, njeo na hali na kadhalika. Vipengee hivi huipa matini ubora unaofaa.

Katika *Madhabahu ya Kilio,* matukio, wahusika, mandhari, vifaa na kadhalika ni vitu vyenye uhalisi unaopatikana katika dunia anomoishi msomaji. Hadhira ya Kiswahili itayaona mambo haya kuwa karibu sana nayo kwa jinsi yanavyojinasibisha na ulimwengu wa hadhira hiyo. Hii ni jamii ya kawaida ambamo mna matabaka ya viongozi kama kina mheshimiwa Mbagaya na Gasia. Kwa upande mwingine kuna tabaka la raia wa kawaida kama kina Boge, Billy Kanzika, Dora na wengine. Katika jamii yoyote ile, sharti pawe na kundi la wanyonge wasioridhika kimaisha kama vile kina Boge wanaowalaumu Wazungu na viongozi kwa matatizo yanayowakumba. Hawafurahii jumba la madhabahu ya kitaifa ya Kilima kutumiwa tu na Wazungu wenye uwezo wa kisiasa na kiuchumi. Mambo haya yanaonyesha uhalisia ambao unashinikiza ukubalifu wa kazi hii katika hadhira pokezi, hivyo kuibua usomekaji na ufasiri miongoni mwa hadhira pokezi. Hii ndiyo dhima ya fasihi kwamba inafaa kushughlulikia maswala yenye uhalisia. Matini tafsiri ya kifasihi ikichunguzwa kwa mujibu wa lugha na fasihi pokezi huweza kuonyesha uamilifu huu kama unavyojitokeza katika *Madhabahu ya Kilio.*

Kifo kwa binadamu ni jambo la lazima tofauti na kuzaliwa ambayo kwa kweli ni bahati. Kifo kinapotokea, sherehe za mazishi pamoja na ada zinazoandamana na mazishi hayo huandaliwa hatimaye mfu akazikwa. Kanaya alipokufa, taratibu zote za maombolezo na maziko zilifanywa. Jamii

ilishiriki kama ilivyo desturi katika sherehe kama hizi. Yapo mapenzi na ndoa kama inavyofanyika kwa Boge na Kanaya na baada ya kifo cha Kanaya, kunakuwa na ndoa kati ya Boge na Kamonya. Haya na mengine mengi ni baadhi ya mambo yanayoshuhudiwa na binadamu katika maisha yake hivyo yakielezwa kwa binadamu ambaye ni hadhira lengwa, yanaeleweka. Endapo lengo la matini tafsiri linaepuka uhalisia uliomo katika matini asilia, inabidi msomaji kuibua usomaji na ufasiri kulingana na uhalisi wa mambo katika ulimwengu wake. Kwa hivyo, tafsiri ni mabadiliko muhimu yanayoibua uhalisi wa maisha. Uhalisi huu ndio unaoipa matini husika kiasi cha ubora unaoshinikiza kukubalika kwayo katika mfumo pokezi.

Maswala ya siasa yameelezwa kwa kugusia mambo kadha wa kadha. Kwa mfano, inasemekana;

> Kama ilivyo desturi katika mazishi, mbunge wa sehemu fulani hangeweza kuhudhuria mazishi ya mtu wa sehemu hiyo bila kuombwa azungumze maneno machache (uk 156).

Mbunge ni mwakilishi wa kisiasa wa eneo fulani ambaye huwasilisha malalmishi ya watu wa eneo analoliwakilisha. Jambo hili lina uhusiano na maudhui ya uongozi. Tunaambiwa na mzungu katika baa wakati Boge anamkataza kuwapiga picha wanawake wakiwa uchi. Anasema hivi;

> Bwana we, unasema nini? Hutaki wapate chakula? Mimi sikuleta ukosefu wa kazi katika nchi ya Kilima. (uk 97)

Hapa, msomaji anahusisha usemi huu na suala la umiliki wa nyenzo za uzalishaji mali kwa mzungu ambapo Wakilima wanabaki katika hali duni katika nchi yao wenyewe. Msomaji anayezifuata fununu za aina hii katika matini, ataweza kuibua ufasiri unaoaminika kwa mujibu wa taratibu za lugha

pokezi zilizotumiwa na mtafsiri. Hivyo swala zima la ubora wa maandishi linajikita katika matumizi bora ya taratibu za lugha husika pamoja na uhalisi wa mambo yanayojadiliwa na kuafikiwa kwa lengo la mtafsiri.

### 3:4:3 Kaida ya uhusiano

Kaida hii hutambulika katika matini kwa jinsi vipengele fulani vinahusiana moja kwa moja na maudhui makuu ya matini. Msomaji wa matini iliyotafsiriwa anafaa kuvibaini vipengele vya namna hiyo ndipo kazi iweze kusemekana kuwa inasomeka hasa kwa msomaji aliyenuiwa. Kaida hii ya uhusiano inadai kuwa, msomaji aweze kutambua wazi maudhui ya kazi anayoisoma. Kwa hivyo, tunaporejelea maudhui ambayo tumeyazungumzia katika shehemu ya yaliyomo, tunaona kuwa mtafsiri ametimiza kaida hii. Kule kutaja mambo ya utamaduni kama vile moto maalumu wa maombolezi, mtu kuzikwa mahali ambapo kiunga mwana chake kilizikwa, na kadhalika ni mambo yanayohusiana na maudhui anayoyashughulikia ya utamaduni.

### 3:5.1 Mwingiliano matini

Mwingiliano matini ni dhana yenye maana ya uhusiano baina ya matini fulani na matini nyingine. Haiwezekani kuwa na kazi ambayo imeibuka tu katika ombwe bila kuhusishwa na kazi nyingine tangulizi. Waandishi huathiriana kwa namna nyingi na hivyo unapata kuwa, katika kazi fulani vipo vipengele mbalimbali ambavyo vinaonyesha uhusiano na kazi nyingine kama hizo. Mwingiliano matini ni dhana yenye sifa ya ubia kwa maana zipo taratibu fulani ambazo huhusishwa na kazi fulani ya kisanaa katika ulimwengu mzima.

Kimsingi, matarajio ya msomaji katika matini pokezi yanahusishwa na matini asilia za lugha pokezi. Kwa mfano, ikiwa matini imetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi ya Kiswahili, msomaji wa tafsiri anatarajia kukumbana na taratibu zile zile zinazopatikana katika matini asilia za Kiswahili. Hivyo, mtafsiri ana jukumu la kuiunda matini yake kwa kufuata taratibu za kiisimu zinazotambulika kwa msomaji huyu wa Kiswahili. Hapa ndipo dhana ya mwingiliano matini inapotumiwa. Kwamba matini iliyotafsiriwa husomeka na kueleweka kwa sababu zipo matini tangulizi zinazoshabihiana nayo katika daraja kadha wa kadha. Daraja hizi zinaweza kuwa maudhui, usawiri wa wahusika, malengo na dhamira za kimaandishi. Kuhusu hoja hii, Neubert na Shreve (1992) wanasema;

> Matini tafsiri mara zote huingia katika mahusiano ya aina mbali mbali na matini asilia za lugha lengwa. Sharti matini tafsiri ihisike na isomeke kama zile za kiasilia (Uk 118).

Wanachokisema Neubert na Shreve ni kuwa matini haiwezi kuepuka ule mwingiliano na matini nyingine tangulizi. Hii ni kwa sababu tafsiri hufanywa kwa sababu kuna uhitaji katika jamii pokezi; uhitaji wa ujumbe ulio katika matini asilia. Hivyo watafsiri huwa ndicho kiunzi kati ya matini asilia na matini lengwa. Hali hii ndiyo hupelekea matini tafsiri kusomwa na kufasiriwa katika jamii pokezi kama kwamba ni matini asilia ya lugha yao.

Mwingiliano matini hubaini taratibu mbalimbali za kiisimu ambazo hutumiwa katika matini mbalimbali. Pia hali ya mwingiliano matini hutambulika katika misingi ya uainishaji wa matini. Kwa mfano, matini za kisayansi zitakuwa na vipengee sawa vinavyozibainisha kutoka kwa matini za kifasihi. Vile vile, katika fasihi vipo vipengee vinavyozibainisha tanzu mbalimbali na ambavyo hupelekea hali ya mwingiliano matini kuonekana

katika matini. Kwa mfano, riwaya iliyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili, inatarajiwa kusawiri vigezo vya kuitambulisha riwaya ya Kiswahili kwa hadhira ya Kiswahili. *Madahabahu ya Kilio* ni matini iliyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza na si ajabu imesawiri taratibu za kawaida za riwaya za Kiswahili kama vile maandishi ya kinathari, masimulizi, uhalisia wa mambo na mengine hivyo kuweza kusomeka na hadhira hiyo kama riwaya ya Kiswahili.

*Madhabahu ya Kilio* imejitokeza kama riwaya kwa jinsi ilivyotumia lugha kinathari. Haya ni masimulizi ambayo yanatoa hadithi ambayo ndiyo msingi wa riwaya. Yupo msimulizi ambaye anasimulia hadithi katika nafsi ya tatu kisha kumpisha mmoja wa wahusika kusimulia baadhi ya sehemu za hadithi hiyo katika nafsi ya kwanza. Mpishano huu ni mbinu ambayo licha ya kutumika katika tafsiri hii haijitokezi kwa mara ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili. Imewahi kutumika katika riwaya nyingi zilizotungwa asilia katika lugha ya Kiswahili. Kwa njia kama hii, kazi inayotafsiriwa haiwi kitu kigeni au kioja kisichojulikana, badala yake inapokelewa kama kiungo katika mfumo mzima wa fasihi pokezi au utanzu maalumu wa fasihi pokezi.

Kwa upande mwingine, riwaya hii imesawiri uhalisia ambao unajitokeza pia katika kazi nyingine nyingi za kifasihi katika lugha ya Kiswahili na hata katika lugha ya Kiingereza. Uhalisia huu ni kiunzi muhimu cha kumshikamanisha msomaji na matini. Uhalisia ni kipengee muhimu cha riwaya. Kwa mfano, maswala yanayoshughulikiwa ni mambo ambayo hadhira pokezi imekumbana nayo katika kazi nyingine za kifasihi zilizotangulia. Maswala ya ukoloni mamboleo, utamaduni, ubadhirifu, kutowajibika kazini kwa Mwafrika, nafasi ya wanawake, uzindushi wa jamii na kadhalika ni mambo ambayo yameangazwa mno katika fasihi ya Kiswahili hasa baada ya ukoloni.

Tamthilia kama, vile *"Kilio Cha Haki"* ya Ali Mazrui, *"Mashetani"* ya Ibrahim Husein, *"Visiki"* ya Khaemba Ongeti na nyingine nyingi zimeshughulikia swala la ukoloni mamboleo kwa kina. Riwaya nyingine kama vile, *"Mwisho wa Kosa"* ya Zainab Burhani, *"Kiu"* ya Said M. na kadhalika vile vile zimeshughulikia kwa undani mambo ya nafasi ya mwanamke katika jamii ya Kiafrika. Haya yote ni mambo yanayomgusa msomaji kwa jinsi yanavyoshabihiana na ulimwengu halisi anamoishi. Aghalabu, unaposoma matini yoyote ile na kupata kuwa yaliyomo si mapya, basi hilo huwa shinikizo kwako kuendelea kusoma na kupata mafunzo muhimu katika maisha. Kwa njia nyingine, kubainika kwa aina hizi za maudhui ni jambo linalowezesha usomekaji na ufasiri wa kazi tafsiri kwa mujibu wa kaida, matarajio na taratibu za lugha pokezi.

Katika *Madhababu ya Kilio,* tunampata mhusika kijana Boge ambaye anawakilisha vijana wa Kiafrika ambao wamesoma na kuzinduka. Kuzinduka kwa namna wanavyoyaona mambo kwa uangavu zaidi na kujaribu kuwazindua Waafrika wenzao. Amegundua kuwa baada ya Ukoloni katika nchi ya Kilima, viongozi waliochukua hatamu waliiga na kuendeleza mbinu za utawala za wakoloni. Anatufunulia kisa cha sera ya utamaduni ambayo iliwahi kuwashirikisha Wakilima kuiunda lakini ikafa bila kutekelezwa. Ndoto ambayo humjia kila mara inadhihirisha wasiwasi wake juu ya utamaduni wa Kiafrika unaozidi kudidimizwa huku mti wa uzungu ukizidi kumea ndani ya Waafrika na jambo hili humuogofya. Wakati wa mazishi ya Kanaya huko Seboa, ndiye mhusika aliyekerwa mno na jinsi nyanyake Kanaya alivyotendewa alipojaribu kupinga maamuzi ya Mheshimiwa. Bila shaka Boge ameonyesha kuwa anapinga jinsi watu wanavyowahusudu viongozi. amejitokeza kama mzindushi wa jamii anaposema;

Tunachohitaji kwa dharura ni sera kamili ya utamaduni na Wakilima wachanga wenye ujuzi na waliojitolea kuitekeleza kikamilifu sera hiyo hadi mwisho wake (uk 29).

Hali hiyo imejitokeza katika kazi nyingi tangulizi katika fasihi ya Kiswahili jambo ambalo ndilo zao la hali ya mwingiliano matini katika riwaya hii. Ni jambo ambalo msomaji wa matini pokezi ameshakumbana nalo katika matini nyingine hivyo kumwezesha kuisoma kazi hii na kuikubali kama mojawapo ya kazi za kifasihi katika lugha pokezi. Hivyo, mtafsiri anachangia fasihi ya Kiswahili kwa kuliendeleza jambo hilo, kulipa ufasiri mpya au hata kulifikisha katika upeo mpya na wa juu wa uelewa na uzalishaji wa maarifa mapya.

Katika tamthilia ya *'Mashetani'* kuna kijana msomi ambaye ni Kitaru anayehusika kama mzindushi. Wasiwasi wake ni kuwa kuna mwanya mkubwa kabisa kati ya matabaka; tabaka la viongozi matajiri na tabaka la maskini. Angependa hali hii ibadilike. Katika tamthilia ya *'Kilio cha Haki'* kijana wa kike Lanina amepewa nafasi ya kuzindua jamii vile vile kuonyesha kuwa mwanamke yu mbioni kujinasua kutoka kwa minyororo ya utamaduni unaomkandamiza. Hali hii inapatikana katika *Madhabahu ya Kilio* pale ambapo wasichana kama Kanaya, Kamonya, binti Gasia wanajikakamua na kufikia kiwango cha juu cha masomo.

Zipo baadhi ya tafsiri ambamo kuna uwezekano wa maandishi ya lugha chanzi kupatikana katika matini tafsiri. Hali hii hupelekea miundo ya lugha ya matini chanzi kujitokeza katika matini pokezi. Hivyo mwingiliano wa matini husababisha mwingiliano wa lugha. Kwa mfano baadhi ya mabadiliko ambayo hutokea katika lugha huweza kuletwa na athari ya matini chanzi kwa

matini pokezi. Neubert na Shreve (1992) wanatupatia mfano wa Kiingereza cha kale kilivyoathiriwa na Kilatini kupitia kwa tafsiri. Wanasema hivi;

> Kama mfano, zingatia jinsi kutafsiri matini za Kilatini hadi Kiingereza cha kale kulivyopelekea kubuniwa kwa maumbo mapya ya kisarufi na ya kileksika pamoja na ukopaji wa maneno (Uk 121).

Hivi ndivyo lugha nyingi zinavyopitia mabadiliko ya aina mbalimbali kupitia kwa tafsiri kwa sababu ya ule mwingiliano matini.

Vielekezo vingine vya mwingiliano matini ni matumizi ya vipengee vya tanzu nyingine tofauti katika kazi husika. Katika matini moja kunaweza kupatikana matumizi ya nyimbo, vipengee vingine vya lugha ya kishairi, tamthilia, hadithi fupi, na kadhalika. Umuhimu wa kuchanganya sifa za tanzu hizi ni kuwa; sifa za tanzu hizi zinawezesha usomekaji mpana na hivyo mwingiliano mpana na kazi tangulizi. Baada ya kusoma maelezo marefu ya kinathari, msomaji hupata shauku kubwa ya kusoma anapokumbana na mtindo wa mazungumzo ya kidrama, ushairi, nyimbo na kadhalika. Aghalabu matumuzi ya mbinu hizi za uandishi hueleza mawazo mazito yenye umuhimu katika matini nzima. Kwa kufanya hivi, huweza kuteka makini ya msomaji na kuifanya kazi kusomeka na kufasirika. Mazungumzo haya yanayopenyezwa katika maelezo ya kinathari huonyesha mijadala ambayo huonyesha tofauti za kimtazamo. Kwa mfano, inaweza kuwa mijadala baina ya vizazi tofauti, au jinsia tofauti au hata vyama vya kisiasa. Tofauti hizi zitajitokeza katika mazungumzo ya wahusika wenyewe hivyo kumgusa msomaji kihisia hivi kwamba anajihisi yu karibu sana na wazungumzaji. Hali hii basi huchangia sana usomekaji wa kazi husika.

Katika riwaya ya *Madhabahu ya Kilio* tunapata kuwa kuna mwingiliano wa kimatini na tanzu nyingine. Mwingiliano huu unajitokeza katika mtindo uliotumiwa kwani kuna sehemu ambayo imeelezwa kitamthilia.

Boge anapomhoji Mhe. Gasia, mtindo ni wa kitamthilia ambao tayari umeingiliana na masimulizi ya kawaida. Katika fasihi ya Kiswahili, zipo tamthilia nyingi na ambazo zimeshughulikia maswala yanayogusiwa katika sehemu hii. Kwa sababu hii, hadhira inakumbana na mtindo iliyowahi kukumbana nao katika tamthilia za Kiswahili; jambo ambalo linawezesha usomekaji na ufasiri. Mifano ya tamthilia kama hizi ni kama vile tamthilia ya kiubwege ya *Amezidi*, inayojikita katika matatizo ya bara la Afrika ukiwemo umaskini, elimu duni, ubadhirifu na kadhalika. Katika sehemu ya mazungumzo kati ya Boge na Mhe. Gasia, swala la ubadhirifu wa mali ya umma unajitokeza.

Ushairi na nyimbo pia zimetumiwa kama mbinu mojawapo ya uandishi katika riwaya hii. Mtafsiri amejaribu kuzingatia mbinu hizi zinazotumiwa sana na wasanii kama vipengele vya mwingiliano matini. Katika (uk 142) kuna ushairi wa Minayo akimkariria dadake ambaye ni Nyamusi nyanyake Kanaya.

Jambo muhimu linalosisitizwa na shairi hili linahusiana na swala la kifo ambalo ni mojawapo wa maudhui ya riwaya hii. Ni kwamba kifo hakizuiliki na binadamu hana uwezo juu ya kifo. Kifo kimemchukua Kanaya ambaye ni kijana anayetegemewa na nchi kwa maendeleo yake katika nyanja mbali mbali ilhali Nyanyake mwenye umri mkubwa yu hai. Tunapata kuwa, waandishi wengi wa nyakati hizi za baada ya ukoloni wamejaribu kuliingilia swala la maisha yalivyokosa maana na jinsi binadamu hana hiari kwa kifo. Msomaji wa *Madhabahu ya Kilio* anatarajia mambo haya kushughulikiwa kwa sababu ni mambo ambayo yamo katika kazi nyingine zilizotangulia. Matarajio haya ni zao la mwingiliano matini ambapo katika uwanja wa fasihi

hakuna mwandishi anayeandika katika ulimwengu wake pekee yake bali huathiriwa na waandishi na kazi tangulizi.

# SURA YA NNE

## MAHITIMISHO

Utafiti wetu katika kazi hii umejishughulisha na vipengele vinavyochangia na kuhimili usomekaji katika *Madhabahu ya Kilio*. Hii ni kwa kuwa ni imani yetu kwamba msingi bora wa kusoma na kufasiri kikweli kazi iliyotafsiriwa unatokana na uzito wa mawazo na uyakinifu wa kile kinachosemwa pamoja na jinsi kinavyosemwa. Kazi hii, tofauti na zilivyo kazi zilizotangulia katika kuchunguza suala zima la tafsiri katika fasihi ya Kiswahili, imejishughulisha na kuonyesha jinsi matini tafsiri inavyoweza kusomwa na kufasiriwa katika upekee wake bila kuifungamanisha na matini asilia. Mkabala huu wa kushughulikia kazi za tafsiri ni mkabala mpya na unaokwenda kinyume na mikabala ya awali iliyoegemea kwa kiasi kikubwa katika utetesi wa kuzitetea haki na kanuni za kijumla za matini asilia; lugha yake na malengo yake. Katika uchunguzi tulioufanya, tumechukua mwelekeo unaowezesha usomaji wa tafsiri kwenda hatua nyingi zaidi ya kuorodhesha makosa ya kiisimu na kisarufi. Mwelekeo huu, tunaweza kudai unaipa matini tafsiri nafasi ya mbele kabisa kwa mujibu wa hadhira pokezi.

Pamoja na mambo ya kimsingi kabisa ambayo tumeyaonyesha ni jinsi usomekaji wa matini tafsiri unavyoweza kuchunguzwa kwa kuzingatia matumizi ya taratibu za kiisimu za lugha pokezi, tumeonyesha kwamba makosa madogo madogo ya kiisimu na kisarufi hayainyimi kazi tafsiri usomekaji. Kwa kujikita katika matini pokezi, tumejaribu kuonyesha kwamba kinachotafsiriwa katika tafsiri za kifasihi si mifumo na masharti ya kiisimu bali maudhui na mawazo ya kijumla ya kazi asilia. Hii ndiyo maana mtafsiri huwa anawajibika kwa msomaji na hivyo analazimika kuutambua ujumbe

muhimu ambao ataufikisha kwa hadhira pokezi kwa kutumia lugha na kaida za upokezi za lugha pokezi. Hii ndiyo sababu ya kimsingi kabisa ambayo inatufanya kuchunguza usomekaji wa *Madhabahu ya Kilio* kwa kumzingatia msomaji katika lugha ya Kiswahili, matakwa na matarajio yake kwa kufungamana na matakwa, kanuni za kiisimu na kaida za kimatini za lugha ya Kiswahili. Ikiwa matini tafsiri zitaendelea kuchunguzwa katika misingi ya miundo ya kisintaksia, kisemantiki na kaida za kimatini za lugha chanzi, basi inaweza kuhitimishwa kuwa tafiti za aina hiyo haziwezi kuifaidi hadhira ya Kiswahili. Kwa kuwa bado tafsiri zinahitajika na zitaendelea kuwepo, ipo haja kukubali mikabala mipya ya kushughulikia na kutafiti fasihi tafsiri, hasa ile mikabala inayomtambua na kumpa msomaji wa tafsiri nafasi ya kimsingi.

Katika utafiti huu, tumeona kuwa katika matini ya ***Madhabahu ya Kilio,*** taratibu za kiisimu zimeafikiana na matakwa na matarajio ya hadhira ya Kiswahili. Matumizi ya viunganishi, vipashio vinavyoonyesha njeo na hali, viwakilishi, usambamba, urejelezi na kadhalika vimetumiwa kuipa matini hiyo upatanishi unaofaa kuunda matini. Vipengele hivi vimeipa matini hii nafasi sawa na riwaya asilia za Kiswahili hivi kwamba msomaji asiye na ufahamu wa matini asilia hatatizwi ila tu katika sehemu chache mno ambapo mtafsiri aling'ang'ania kutosheleza au kusukumiza taratibu za lugha ya Kiingereza. Ni wazi kuwa palipo na tafsiri, lugha huwa tofauti na hadhira vile vile ni tofauti na hii ndiyo sababu matini tafsiri haifai kutathminiwa kwa kuifungamanisha na lugha asilia. Sharti mtafsiri afanye mabadiliko ambayo yataishinikizia kazi yake ukubalifu katika mfumo mzima wa wapokezi.

Mabadiliko ambayo mtafsiri hulazimika kufanya ni pamoja na kupunguza au kuongeza maelezo, au hata kuondoa maelezo mengine yasiyoleta maana katika ulimwengu wa hadhira pokezi. Haya ndiyo baadhi ya mambo ambayo yamepelekea kufikiriwa upya suala la tathmini ya tafsiri.

Mielekeo inayopendelewa zaidi hivi sasa ni ile ya kihadhira kuliko ule uaminifu unaoshikamanishwa na matini asilia. Kuna mambo yaliyo ndani ya matini iliyotafsiriwa ambayo ni muhimu kwa hadhira pokezi kama ilivyojitokeza katika utafiti huu. Ujumbe unaotokana na ufasiri ambao msomaji ameuibua unajinasibisha na hali halisi ya maisha ya hadhira pokezi kihistoria, kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kiwakati. Kwa sababu hii, hadhira inaweza kuvutiwa kusoma matini hii na kuifurahia ikiwa hawakupata nafai ya kukumbana na matini asilia.

Kwa mambo haya ambayo tumeyajadili, tumeona kuwa kazi tafsiri hutoa mchango kwa lugha na fasihi pokezi kwa njia mbalimbali. Na kwa hivyo, mtafsiri ni mwanasanaa yaani mwandishi anayezalisha na kuingiza katika fasihi pokezi mafunzo, maadili na maarifa mapya. Mwelekeo huu wa kulichunguza swala zima la tafsiri unafaa kuzua mijadala ambayo inaweza kupelekea utafiti zaidi wa uamilifu na utimilifu wa tafsiri.

Ni jukumu la wataalam wa Kiswahili kuchunguza zaidi maingiliano ya kitamaduni katika suala la tafsiri. Ningependekeza pia kuwa kaida za mawasiliano na athari zake zifanyiwe utafiti katika matini zilizotafsiriwa ili kubaini uamilifu wake katika mfumo pokezi. Vile vile, lingekuwa jambo mwafaka ikiwa uchunguzi ungefanywa (kwa kuzingatia mwelekeo wa mfumo pokezi) kubaini namna ya tafsiri ambayo inafaa sana kwa matini za kifasihi. Utafiti kama huu utachangia pakubwa somo la tafsiri na kutoa maelekezo kwa watafsiri chipukizi wanaonuia kukuza lugha ya Kiswahili na kuendeleza fasihi katika jamii.

## MAREJELEO


Ali,C.W (1981) *The problems of Translating From English to Swahili as Exemplified by V.O.K. News Items* M.A Thesis.University ofNairobi

Albrecht, N. & Shreve, M. (1992) *Translation as Text* LONDON, The Kent University Press.

Birch David (1989) *Language, Literature and The Critical Practice* LONDON, Routledge.

Brown, G (1983) *Discourse Analysis* CAMBRIDGE, Cambridge University Press.

de Beaugrande, R & Dressler, W (1981) *Introduction to Text Linguistics* LONDON, Longman

Gilliland, J (1972) *Readability* LONDON, Hodder & Stoughton

Grice.H.P (1981) 'Presupposition and Conversational Implicature' in (ed.)P.Cole *Radical Pragmatics.*NEWYORK. Academic Press.

Holbrook Jackson (1949) *The Reading of Books* London, Faber and Faber Ltd

Imbuga Francis (1993) *Shrine of Tears,* NAIROBI, Longhorn Publishers

Ibid (2003) *Madhabahu ya Kilio* NAIROBI, Metro Language and Communication Centre.

Joel, Wingard (1996) *Literature, Reading and Responding to Literature* New York, Harper Collins Publishers.

Newmark Peter (1988) *A Text Book of Translation* UK, Prentice Hall International (UK) Ltd.

Ngara Emmanuel (1982) *Stylistic Criticism & The African Novel.* London, Heinemann Educational Books Ltd.

Rodney, W. (1972) *How Europe Underdeveloped Africa* LONDON, Bogle – L'overture Publications.

Ryanga,C.W (1985) *Vitabu Vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili.Katika Tuki Vol.52.* University of Dar es Salaam.

Sherry S. & St. Pierre, P (2000) *Changing the Terms* OTTAWA, University of Ottawa Press.

Shitemi, Naomi (1990) *Mawasiliano Katika Tafsiri: Uteuzi wa Mtafsiri* M.A Thesis, University of Nairobi.

Thomson, D (1979) *Reading and Discrimination*
London, Chatto and Windus Ltd.

Toury, G (1995) *Descriptive Translation Studies and Beyond*
Amsterdam, John Benjamins Publishing Company.

Tymoczko, M (1999) *Translation in a Post Colonial Context*___MASSACHUSETTS, St. Jerome Publishing.

Zaja,O (1986) *Fasihi Tafsiri Katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili:Matatizo na athari zake.*
M.A Thesis. University of Nairobi.